**Nipashe**

Jumatatu Juni 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580604

www.ippmedia.com

MWANGA WA J

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



**Serikali** yajivunia mafuriko ya wawekezaji miezi miwili

UKURASA 3



**Samia** atoa agizo usafirishaji korosho mikoa mitatu Kusini

UKURASA 5

**Ramos anukia kutua Man Utd**

UKURASA 20



# Kifo cha TB Joshua chawashtua wengi

• **Mamia** waomboleza mtandaoni, waumini wake wajaa nje ya kanisa...*Endelea ukurasa 19*

# Kipimo cha corona chaibua malalamiko uwanja wa ndege

UKURASA 2



Baadhi ya wageni waingiao nchini wakiwa katika mstari Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam wakisubiri kupatiwa namba za kulipia huduma ya kupimwa Corona. **MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**NCCR YAONA MATUMAINI MAPYA KWA RAIS SAMIA**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimesema kimeona matumaini mapya ya Rais Samia Suluhu Hassan...

**UKURASA WA 5**

**91 MBARONI KWA TUHUMA ZA UJANGILI**

MAMLAKA ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kanda ya Magharibi, imewakamata watu...



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, akimkabidhi Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Edwin Mhede Ripoti ya mwaka ya utendaji kwa mwaka 2020 baada ya kumaliza mkutano mkuu wa mwaka makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mwanasheria Mkuu wa benki hiyo, Lilian Komwihangiro na kulia ni Ofisa Mkuu wa Fedha, Juma Kimori. **Habari ukurasa 8. MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Dunia yaipa Tanzania trilioni 2.3/-

UKURASA 2

**MICHEZO** **CHIRWA ANOGEWA LIGI KUU BARA** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe (kulia), akimsikiliza Afisa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Waziri Ramadhan (wapili kushoto), wakati alipotembelea banda la UTT AMIS kwenye maonyesho na maadhimisho ya Wiki ya Unywaji Maziwa Kitaifa mkoani Tanga. Wengine ni Kaimu Mkurugenzi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uzalishaji na Masoko, Stephen Michael (wapili kulia) na Afisa Masoko Mwandamizi wa UTT AMIS, Grace Ngailo.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kipimo cha corona chaibua malalamiko uwanja wa ndege

**Na Mwandishi wetu**

WASAFIRI katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, wamelalamikia utaratibu uliopo katika kupata namba, kulipia na kupimwa corona kwa wanaowasili kutoka ughaibuni.

Hali hiyo kwa wasafiri imekuwa kero kiasi cha baadhi kuachwa na ndege, kukaa zaidi ya saa tatu hadi nne bila huduma.

Aidha, muda mwingi wasafiri wanautumia kusubiri utaratibu wa kupata namba, kulipia na kupata fomu ya kupima.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imethibitisha kupokea malalamiko ya wasafiri na kufafanua hali hiyo ilisababishwa na maboresho yanayofanyika kwenye kulipia mtandaoni na kukosekana mtandao.

Majira ya saa nane usiku hadi saa 10 juzi ziliwasili ndege nne za Shirika la Ndege Ethiopia, Shirika la Ndege la Kenya (KQ), Shirika la Ndege la Ethiopia na Shirika la Ndege la Uturuki, kila mmoja likiwa na abiria wengi.

Abiria hao walitakiwa kupanga foleni, huku wakiingia kwenye mfumo wa Wizara ya Afya, uitwao 'Afya Msafiri' kwa ajili ya kujaza fomu na kupata namba maalum ya malipo.

Katika eneo hilo kuna wahudumu watatu ambao anahudumia abiria wote (wastani wa watu 500) waliopanga foleni ambao wanatakiwa kuwa na namba ya kulipia, ambayo lazima ihakikiwe ndipo msafiri aruhusiwe kwenda kupima.

Aidha, abiria wote wenye watoto, wajawazito, wenye ulemavu, waliokaa kwenye viti mwendo, wazee, wagonjwa na wazima wanapanga foleni moja, huku kutokana matatizo ya mtandao wanasimama kwa muda mrefu.

"Nimewasili na Ndege ya Ethiopia tangu saa nane kasoro na nimesimama kwenye foleni kwa zaidi ya saa mbili bila huduma, wanasema hakuna mtandao wa kuhakikisha kama namba ya kulipia niliyopata ni sahihi, lakini hakuna utaratibu sasa kila mtu anapita atakavyo, hakuna matangazo juu ya utaratibu kiasi sasa cha kuwa mwenye nguvu apite,"nalisema mmoja wa wasafiri.

"Kama unavyoona ndege nyingine imewasili na abiria waongezeka na wote tunasubiri huduma hii, huu utaratibu unaumiza wengi, na sasa tunaelezwa mtandao haufanyikazi," aliongeza.

**MTANDAO KUSUMBUA**

Kwa mujibu wa msafiri huyo, baada ya kukaa kwa saa mbili ndiyo alipata huduma ya namba kuangaliwa kuwa iko sawa baada ya mtandao kurejea, na alipofika pa kulipia alishindwa kufanya hivyo kutokana na mtandao.

Aidha, wasafiri waliokuwa wanalipia kwa kadi za VISA alishindwa kufanya hivyo na hata waliosimama kwenye dirisha la benki inayotoa huduma eneo hilo alishindwa kupata huduma na kulazimika kusubiri kwa saa moja nyingine.

Pia, wasafiri wengi walijaziwa fomu za malipo kwa mkono kwa madai mtandao hauwezi kutoa nakala ya fomu ambayo mteja anatakiwa kupewa.

Mara baada ya kulipia msafiri anatakiwa kwenda kwa wahudumu wa afya, ambao humjazia fomu maalum ya kumruhusu kwenda kupima ambako napo kulikuwa na tatizo la mtandao.

Baadhi ya wasafiri ambao walikuwa anabadili ndege walijikuta wakitumia muda mwingi kwenye utaratibu huo na baadhi kushindwa kuwahi ndege za ndani za kuelekea Arusha, Mwanza na Kigoma.

Kwa upande wa wahudumu walikuwapo watatu ambao wanaangalia namba na pasi za kusafiria za wasafiri kabla ya kuwaruhusu kulipia.

Katika eneo hilo daftari linalotumika ni moja kurekodi taarifa za wasafiri na kuwapa namba za kwenda kupima, ambao hutumia chini ya dakika tano kupimwa na kupata majibu, na baadaye kwenda kuvuka mpaka ili kuchukua mizigo.

**UFAFANUZI WA WIZARA**

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mkurugenzi wa huduma za kinga, Dk. Leonard Subi, alisema changamoto zilizojitokeza juzi ni kutokana na mtandao, na kwamba wamefanya mabadiliko ya mtandao ili msafiri aweze kujaza fomu na kulipa kabla ya kufika nchini.

"Tumepokea malalamiko ya kilichotokea jana (juzi) usiku kuwa ziliwasili ndege nne kwa wakati unaofuatana na kulikuwa na shida ya mtandao kuanzia kwenye kuhakikisha namba ya malipo, malipo na kujaza fomu, tumechukua hatua,"alisema.

Dk. Subi alisema kwa mtandao uliobadilishwa inatakiwa msafiri kukamilisha utaratibu wote ndani ya dakika 10 hadi 15, lakini kwa kuwa tupo kwenye kipindi cha mpito ndiyo maana usumbufu ulijitokeza.

Aidha, alisema serikali ilianzisha utaratibu wa kupima tena mara msafiri anapowasili kutokana na kuwapo vyeti vya COVID-19 vya kughushi,huku wengine wakipata maambukizi wakiwa safarini na kuingiza nchini.

**TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI**

**ANTHONY NELSON KAFUGUGU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA PIAGGIO APE YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 890 BQH NA** CHASSIS NO. **MBX0002CFUB418339.** ENGINE NO **TBPDMBU3002221.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA **POLISI KAH/ TR /RB/577/2020.**

# WB yaipa Tanzania mkopo zaidi tril. 2/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BODI ya Wakurugenzi ya Benki ya Dunia imetoa mikopo minne ya masharti nafuu kwa Tanzania yenye thamani ya Sh. trilioni 2.33 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Dk. Nchemba alisema awali bodi hiyo iliidhinisha mikopo mitatu yenye masharti nafuu ya Sh. trilioni 2.012 kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maendeleo.

Hata hivyo, Juni 3, mwaka huu, bodi hiyo tena iliidhinisha mkopo mwingine wenye thamani ya Sh. bilioni 326.6.

"Hatua hiyo imefanya jumla ya mikopo yenye masharti nafuu iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Dunia kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia minne ikiwa na thamani ya Sh. trilioni 2.3391," alisema.

Alisema mikopo hiyo itatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo wa Roads to Inclusion and Socio -economic Opportunities (RISE), wenye mkopo wa Dola za Marekani milioni 300.

"Miradi mingine ni Higher Education for Economic Transformation Project (HEET), wenye mkopo wa Dola za Marekani milioni 425, mradi wa Digital Tanzania Project (DTP) wa dola milioni 150 na mradi wa Zanzibar Energy Sector Transformation and Access Project wa dola milioni 142," alisema Dk. Nchemba.

Pia, alisema mradi wa RISE utasaidia kuboresha barabara za vijijini na kutoa fursa za ajira takribani 35,000 kwa wananchi katika vijiji nufaika pamoja na kujenga uwezo wa usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kuhusisha njia shirikishi za jamii.

"Mradi huu utahusisha ujenzi wa jumla ya kilometa 535 kwa kiwango cha lami katika wilaya sita za mikoa ya Iringa, Lindi, Geita na Tanga na ukarabati wa maeneo korofi ya barabara za vijijini nchi nzima," alisema Dk. Nchemba.

Vile vile, alisema mradi wa HEET utasaidia kuimarisha mazingira ya ufundishaji na mafunzo taasisi za elimu ya juu katika fani za kipaumbele cha taifa kwa kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

"Mradi huu pia utapitia upya na kuboresha mitaala ya vyuo vikuu, kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi wengine ili waweze kusimamia elimu ya juu ili kuwa na wahitimu wanaoendana na soko la ajira na kuchangia maendeleo ya nchi na uchumi kwa ujumla," alisema. Kadhalika, alisema mradi wa DTP utasaidia kuongeza upatikanaji wa huduma bora za mtandao wa intaneti na kuboresha huduma za umma kwa kutumia digitali kwa kustawisha ekolojia ya kidigitali nchini, kuhakikisha uunganishaji wa kidigitali kwa Watanzania wote na kuboresha jukwaa la huduma za kidigitali.

"Pia kuna Mradi wa ZESTA ambao utasaidia kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma bora na za uhakika za umeme visiwani Zanzibar ikiwa ni pamoja na kujenga mitambo yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa kiwango cha MW 18 kupitia nishati ya nguvu ya jua (Solar Power Generation) na msongo wa KV 132 wa kusafirishia umeme katika visiwa hivyo," alisema.

Alisema mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 150 kwa ajili ya mradi wa Boosting Inclusive Growth for Zanzibar (BIG-Z), unategemewa kuwasilishwa katika katika vikao vya bodi ya Benki hiyo Juni 10, 2021 kwa ajili ya kupata idhini.

"Mradi huu utasaidia kuboresha miundombinu ya mijini katika miji ya Unguja na Pemba kwa kujenga na kuboresha barabara za lami, mifumo ya majitaka, mifereji ya maji ya mafuriko, maeneo ya udhibiti mjini Unguja na Pemba ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kukuza utalii katika visiwa vya Zanzibar," alisema, Dk. Mwigulu.

Kuhusu deni la taifa, alisema bado ni himilivu.

# Serikali yajivunia mafuriko ya wawekezaji miezi miwili

**Joseph Mwendapole na Mauld Mbaga**

SERIKALI imesema kuna ongezeko la wawekezaji nchini ambao hadi sasa miradi 59 yenye thamani ya Sh. trilioni mbili imesajiliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC), ndani ya miezi miwili.

Aidha, imesema kutokana na ongezeko hilo, kuna uwezekano wa kuzalisha ajira 12,000 miradi hiyo itakapoanza kufanya kazi

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la Kituo cha Uwekezaji, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Prof. Godius Kahyarara, alisema ongezeko hilo ni kutokana na jitihada mbalimbali zilizofanyika ikiwamo kuondoa vikwazo. Aidha, alisema serikali ina mpango wa kuwa na maeneo huru ya uwekezaji kwa ajili ya kuweka wawekezaji wengi kwenye sehemu moja ili kuwahudumia kwa haraka na kwa wakati.

Alisema sehemu hizo zitawekewa mahitaji yote ya wawekezaji ili kuwawezesha kufanya yale wanayotaka kufanya kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali na kutoa kodi itakayowezesha ukuaji wa uchumi wa taifa.

"Nilikuwa nazungumza na Mkurugenzi hapa kuhusu utekelezaji wa maagizo ya serikali ya awamu ya sita na hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa katika miezi hii miwili...tumebaini kuna mafuriko ya wawekezaji," alisema na kuongeza:

"Tumegundua kwamba tuna mafuriko kwa ababu tunapata barua nyingi sana za watu wanaotaka kuja kuwekeza nchini na hata ukija ofisini kwangu pale utakuta kuna rundo la barua za wawekezaji."

Kwa mujibu wa Prof. Kahyarara, ameshangaa kukuta takwimu za kustaajabisha kwenye kituo hicho ambapo wamefanikiwa kuvutia uwekezaji wenye thamani ya Sh. trilioni mbili kwa miezi miwili pekee rekodi ambayo haijawahi kutokea.

"Hii ni rekodi ambayo haijawahi kutokea na wala sikuwahi kuitarajia kabisa na hii inamaana tukienda kwa mwendo huu kwa mwaka mzima tutakuwa tunazungumzia Sh. trilioni 24," alisema Prof. Kyarara.

Aliongeza kuwa marufiko hayo ni neema hivyo serikali inapaswa kujipanga kuweka mazingira mazuri yatakayowawezesha wawekezaji hao watarajiwa kufanya shughuli zao bila vikwazo, hali ambayo itavuta wawekezaji zaidi.

# NCCR yaona matumaini kwa Samia

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimesema kimeona matumaini mapya ya Rais Samia Suluhu Hassan, huku kikishauri serikali mambo kadhaa ili kuleta usawa na kufikia matarajio ya kukuza uchumi wa taifa.

Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia, akizungumza jana katika makao makuu ya chama hicho Ilala jijini Dar es Salaam, alisema wamekuja na hoja hizo nne ili kukuza mtazamo wa pamoja katika taifa kuhusiana na masuala mbalimbali yanayoendelea nchini.

Alisema mahitaji makuu ya Rais Samia ni kulinda utu katika mazingira yanayomzunguka pia mifumo inayozingatia afya na elimu bora, inayowezesha kutambua na kutumia utajiri uliomo nchini, ili kutengeneza fursa.

Kuhusu uchumi, alisema usalama wa uhai wa wanajamii unategemea hali ya uchumi wa jamii husika, hivyo mfumo uliopo unategemea mzunguko wa fedha ambao kwa sasa ni mdogo hivyo kuwaweka watanzania shakani.

"Rai yetu kwa bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wawe na utashi wa kupitia bajeti itakayozingatia kwamba kipaumbele namba moja ni usalama na uhai wa kila mtanzania, bajeti iwe ya kutuunganisha na kwa kupunguza tofauti zetu kwenye mahitaji muhimu ya misingi ya mwanadamu."

**KUPOTEA KWA LESENI**

**Primus Revelian Laurent** amepoteza leseni za uchimbaji wa madini namba **0392TNG,0393TNG,0394TNG, 0395TNG** na **0396TNG.**Taarifa imefunguliwa kituo cha Polisi Kyaka Wilayani Missenyi jalada namba **KAG/KYA/RB/226840/2021**. Atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES
P.O.BOX 429 DODOMA - TANZANIA
OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9
0715170553 / 0756011439

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Amri ya **Mahakama ya Mwanzo Chamwino Mjini,** wilaya ya Dodoma nitauza mali ya **YAZID IDDY** ambayo ni Nyumba moja iliyo kwenye Kiwanja chenye vipimo **(wu-178-806511, 9322484, wu-570-806496, 9322452, wu-813-806490, 9322454)** Mpamaa Kata ya Miyuji ili kufidia deni analodaiwa na **JOHARI SELEMAN.** Mnada utafanyika Nyumba ilipo na itauzwa kama ilivyo siku ya tarehe 18/06/2021 Saa Nne 10:00 asubuhi.

**MASHARTI YA MNADA KISHERIA**

- Mnunuzi atalipa asilimia 25 (25%) ya bei papo hapo na asilimia 75 (75%) atailipa ndani ya siku 14.
- Mnunuzi akishindwa kulipa asilimia 75 ndani ya siku 14, mnada utarudiwa (utatangazwa upya) na asilimia 25 haitarudishwa.
- Mnunuzi anarusiwa kufika eneo nyumba zilipo kabla ya siku ya mnada kwa gharama zake, akiambatana na afisa wa mahakama.
- Mnunuzi akishanunua gharama za kubadili umiliki ni juu yake.

**MAWASILIANO simu namba (0735 170 553 COURT BROKER).**

**BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI(CRB)**

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUAHIRISHWA KWA MKUTANO**

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi(CRB)** inasikitika kuwatangazia Makandarasi na wadau wote wa sekta ya Ujenzi kwamba mkutano wa mashauriano wa mwaka 2021 uliokuwa ufanyike tarehe **10 hadi 11 Juni 2021** katika ukumbi wa **Gold Crest Mwanza** umeahirishwa, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Bodi.

Mkutano huu sasa utafanyika **tarehe 17 hadi 18 Juni 2021,** katika ukumbi wa **Gold Crest Mwanza kuanzia saa 2 asubuhi.** Kauli mbiu ni: "Juhudi za Makusudi za Wadau Kuwezesha Ukuaji wa Makandarasi wa ndani"

Ada ya ushiriki ni **TZS 50,000/=** kwa Makandarasi na **TZS 100,000/=** kwa Wadau wengine.

Malipo ya ada ya ushiriki yafanyike kwa benki ya **CRDB Plc au NBC ltd au NMB Plc** kwa jina la **CONTRACTORS REGISTRATION BOARD** pia kwa kupitia mitandao ya simu kwa kutumia **"Control number 995740032000"** kwa Makandarasi na **"Control number 995740032001"** kwa Wadau wengine.

Bodi inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

Kwa taarifa zaidi tafadhali usisite kuwasiliana na ofisi za Bodi (Makao Makuu na ofisi za kanda). Atakayeona tangazo hili amtaarifu na mwingine.

**Imetolewa na:**
**MSAJILI**

**Head Office**
P.O.Box 13374, Dar es salaam,
Pamba Road, Tetex House, 3rd Floor,
Tel: +255-22-2137962-3,
Fax +255-22-2137964,
Email: **crbhq@crbtz.org**

**Southern Zone**
P.O.Box 1690, Mbeya,
NHIF Tower 3rd Floor,
Tel: +255-25-2502480,
Email: **crbsz@crbtz.org**

**East Zone**
P.O.Box 33621, Dar es salaam,
Keko Mwanga- Nyerere Road,
Mpingo House, 5th Floor,
Tel: +255-22-2771877/27017,
Email: **crbez@crbtz.org**

**Northen Zone**
P. O.Box 16795, Arusha,
NSSF Mafao House, 11th Floor,
Tel: +255-27-2547107,
Email: **crbnz@crbtz.org**

**Lake Zone**
P.O.Box 2815, Mwanza,
Station Road, Tanroad Compound,
Tel: +255-28- 2500218/2502212,
Email: **crblz@crbtz.org**

**Central Zone**
P.O.Box 2618 Dodoma,
Udom Road,
PSPF Plaza, 1st Floor,
Tel: +255-26-2966040/1
Email: **crbcz@crbtz.org**

# Moto unavyoitesa hifadhi Mlima Kilimanjaro

**Na Jenifer Gilla**

NI kilomita 45 kutoka Moshi mjini, sawa na mwendo wa takribani nusu saa kwa usafiri wa gari na kuukuta Mlima Kilimanjaro.

Mlima huu unaojizolea sifa ya kuwa mrefu kuliko yote barani Afrika na wa pili duniani, ukinakshiwa na miti ya asili ya aina yake pamoja na viumbe hai kama vile mbega, nyani, nyati, chui, tembo, swala na ndege, ambao huongeza vionjo kwa watalii kutoka mataifa mbalimbali wanaokuja kuupanda na kujiwekea rekodi.

Licha ya sifa kubwa iliyonayo mlima huo ulimwenguni, kwa miaka mingi umekuwa ukiandamwa na jinamizi la kuungua moto ambalo linachangia kushusha hadhi yake siku hadi siku.

Nipashe ilifunga safari hadi Makao Mkuu ya Hifadhi ya Mlima huo (KINAPA), Marangu, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro na kufanya mahojiano na mamlaka hiyo kufahamu kinachojiri juu ya suala hilo.

Imani Kikoti, ni Ofisa Uhifadhi Mkuu anayesimamia Idara ya Sayansi na Uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), anayetoa simulizi ya muda mrefu ya hifadhi hiyo kuandamwa na majanga ya moto.

**CHANZO CHA MOTO**

Kikoti anathibitisha katika uchunguzi walioufanya walibaini kuwa hakuna moto wa asili uliotokea katika hifadhi hio, yote husababishwa na shughuli za binadamu.

"Moja ya shughuli zinazosababisha kuzuka kwa moto kwenye hifadhi ni uvutaji wa sigara unaofanywa na watalii pamoja na wasaidizi wao, ambao baada ya kumaliza hutelekeza vipisi vya sigara vikiwa na moto ambavyo husambaa kupitia majani makavu.

Pia, wasaidizi wanapokuwa wakiwapikia watalii chakula, hawazimi moto vizuri wanapomaliza shughuli hiyo na matokeo yake husambaa na kuleta majanga," anasimulia Kikoti.

Sababu nyingine anataja ni uwindaji haramu ambao mwindaji anapokamata mnyama anaamua kumchoma msituni kwa kuhofia kukamatwa kwa kosa la kuwinda bila kibali cha mamlaka.

Anataja pia urinaji wa asali kuwa ni chanzo cha kuzuka moto msituni kwa kuwa wanakjiji wanarina kizamani kwa kutumia moto kufukuza nyuki ambao husambaa na kuunguza msitu.

Njia ya uandaaji mashamba ya kizamani kwa kutumia moto anaitaja kuwa ni chanzo cha moto katika hifadhi kwa mashamba yaliyo karibu na hifadhi hiyo na moto unaochomwa katika mashamba hayo kwa ajili ya kuunguza visiki husambazwa na upepo hadi kwenye hifadhi.



Wafanyakazi wa KINAPA wakizima moto kwenye eneo la Mlima Kilimanjaro.

**ATHARI**

Kwa mujibu wa Kikoti, moto unasababisha kupungua kwa miti katika hifadhi hiyo ambayo ndio tegemeo kuu la kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri dunia.

Mhifadhi huyo anakiri kuwa theruji ya Mlima Kilimanjaro imepungua hadi kufikia kilomita za mraba 1.76 chanzo kikuu kikiwa ni ongezeko la joto linalotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

"Tunategemea miti hii ili kuunusuru mlima kuendelea kuyeyuka na kupoteza mvuto wake, hivyo moto unaowaka kila mara unarudisha nyuma juhudi zetu," anasema Kikoti.

Athari nyingine kwa mujibu wa Kikoti inaangukia kwa viumbe hai wanaotegemea msitu huo kwa makazi ambao hulazimika kukimbia kuhama makazi pale moto unapowaka.

"Mnyama kama ndezi au swala ambao hula majani wanaathirika sana moto unapowaka kwa kuwa wanakosa chakula, kwa hiyo kuhama makazi kutafuta chakula, wengine hutoka nje ya hifadhi kabisa kwa kupitia mashoroba na kwenda kwenye hifadhi nyingine kama vile Serengeti," anasema Kikoti.

Mwenyekiti anena

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msiri, Kata ya Marangu Mashariki, John Mtui, anakiri kuwa moto unapowaka mlimani kunakuwa na hofu kubwa kwa wananchi hali inayosababisha wengine kuondoka kwa muda.

"Unajua kijiji hiki kipo mpakani kabisa na mlima, hivyo moto unapowaka kwa upande wetu huwa tunausikia kabisa hivyo kunakuwa na taharuki na hofu inatawala kuwa huenda unaweza kufika kwenye nyumba zetu usiku na kutuunguza," anasimulia.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa kijiji kwa kushirikiana na idara ya ulinzi na uokoaji ya KINAPA, wanafanya kazi kubwa ya kuwatoa hofu wanakijiji pamoja na kuhakikisha wanachukua kila tahadhari ili moto usifike kwenye makazi ya watu.

"Tunahakikisha hawaendi msituni kipindi chote moto unapowaka ili kuwaepusha na majanga yanayoweza kusababishwa na mto huo," anasema Mtui.

**WANAKIJIJI WALIA**

Katazo la kuingia msituni moto unapowaka hugeuka shubiri kwa wananchi hao ambao hutegemea msitu huo kwa shughuli mbalimbali.

Mesia Robson (31), mkazi wa kijiji cha Msiri analalamika kuwa moto husababisha mifugo yake kukosa chakula na hata kufa kwa kuwa hutegemea kukata majani kwenye msitu huo.

"Kuna mbuzi wangu mwaka jana alizaa watoto wakafa kutokana na kukosa lishe, kwa sababu tulikaa wiki mbili bila ya chakula cha kutosha kwa kuwa moto ulikuwa unawaka msituni," anasema.

Wakati Mary Shayo akalalamikia moto huo kusababisha uhaba wa kuni kwa kuwa hutegemea katika hifadhi hiyo na kusababisha kununua kwa watu ambao huuza bei ya juu.

"Unalazimika kununua kwa walionazo ambapo mtu anakuuzia fungu moja Sh. 2000, kwa kuwa unashida utanunua tu, kwa sisi wenye mahindi ndani tunatumia magunzi.

**ATHARI KIUCHUMI**

Wanakijiji hao pia hulalamikia shughuli za kiuchumi kusimama kutokana na watalii kusitisha kupanda mlima kama anavyosimulia mpagazi Munguatosha Mosha (32).

"Kwa sisi wasindikiza watalii inakuwa ni hatari kwa sababu zile shughuli zinakufa na ndio ajira zetu, na sio kwamba moto ukidhibitiwa tu ndio watalii wanaruhusiwa hapana, hapo mtakaa hata mwezi ili kujiridhisha."

Kwa safari moja inayohusisha siku saba John hulipwa ujira Sh. 100,000 hadi 150,000 kutegemea na kampuni iliyompa kazi.

Alphonce Shayo (35), muuza duka la vitu vya asili katika geti la kupandia watalii la Marangu anasimulia kupata hasara ya takribani Sh. 50,000 kwa siku, moto unapowaka kwenye hifadhi hiyo kutokana na kutokuwapo na watalii wa kuwauzia.

"Huwa ninawauzia vitu vya asili ya Tanzania kama vile shanga, vinyago, picha za mlima, na tunawapatia hapa wanapokuwa wanaelekea kupanda mlimani, sasa kunapotokea majanga ya moto hawaji tena," anasema.

**KILIO HADI SERIKALINI**

Moto huo pia umekuwa ukiitia serikali harasa kwa kuharibu miundombinu pamoja na majengo yalipo ndani ya hifadhi.

Akitoa tathmini ya athari za moto uliotokea Oktoba, mwaka jana katika hifadhi hiyo, aliyekuwa Waziri wa Utalii na Maliasili, Dk. Hamisi Kigwangala, alisema uliteketeza mabanda ya kupumzikia wageni 12, kati ya hayo 10 yakiwa ya wageni wa kawaida na mawili ya wageni maalum ambayo ndio yalikuwa yamekamilika kujengwa kisasa.

Aliongeza kuwa moto huo uliunguza mitambo ya umeme wa jua pamoja na vyoo viwili. Hali itakayoigharimu serikali kuingiza mkono mfukoni na kufanya matengenezo kwenye uharibifu huo.

Naye Mhifadhi Mkuu Kikoti anakiri kuwa majanga ya moto yanaitia hasara serikali kwa kuwa shughuli za utalii zinaposimama kutokana na majanga hayo serikali inakosa pato linalotokana na kodi hiyo.

Kwa mujibu wa mhifadhi huyo, wanapokea wastani wa watalii 5,000 kwa mwaka ambao serikali hupokea kodi kutoka kwa kila mtalii.

Uwapo wa watalii hao pia husababisha kupatikana kwa ajira kwa vijana wa eneo hilo, mhifadhi Kikoti anathibitisha kuwa kila mwaka vijana 2,500 wanapata ajira kwa kuwa kila mtalii mmoja anatakiwa asindikizwe na mpishi mmoja, wapagazi watatu na mwongoza watalii mmoja.

**MABADILIKO YA TABIA NCHI**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Taasisi ya Tathmini ya Rasilimali, Dk. Noah Makula, anatoa ushuhuda jinsi uchomaji wa moto unavyochangia mabadiliko ya tabia nchi akisema:

"Miti inahifadhi hewa chafu inayoitwa 'carbon dioxide sink', inapochomwa hiyo hewa inatoka na kuelekea angani na kuathiri tabaka la ozone, na kuharibika kwa tabaka hili kunasababisha kupenya kwa miale ya joto kutoka angani na kusababisha joto kuongezeka.

Kwa mujibu wa ripoti ya jopo la Wanasayansi wa Utafiti wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), kuhusu athari ya ongezeko la joto, limeongezeka na kufikia nyuzi joto 15, na juhudi za haraka zinahitajika ili kuizuia isifikie nyuzijoto 20.

Wakati huo huo, taarifa za kisayansi zinasema kuwa gesi ya aina ya carbon dioxide (Co2) ndio inaongoza kwa kuathiri tabaka la ozone kwa asilimia 66, ikifuatiwa na methale (CH4) asilimia 15.

**CHANGAMOTO KATIKA UZIMAJI**

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi anayesimamia Idara ya Ulinzi na Uokoaji, Mapinduzi Ndesa, anazungumzia idara yake inapitia changamoto mbalimbali katika kukabiliana na moto unapozuka kwenye hifadhi.

Anataja mojawapo uhaba wa vifaa vya kisasa vya kukabiliana na moto huo ambavyo hufanya shughuli hiyo kuchukua muda mrefu tofauti na matarajio yao.

"Hatuna vifaa vya kisasa vya kuzimia moto vinavyoweza kudhibiti kasi ya moto inayochochewa na upepo, sisi tunatumia magari ya zimamoto, na njia za kawaida za kutumia ndoo za maji na michanga hali ambayo haisaidii kitu.

"Pia hata magari yenyewe yanashindwa kufika eneo la tukio mapema kutokana na changamoto ya njia, kwa sababu kwenye huu mlima kuna sehemu ikifika magari hayawezi kupita inabidi tulazimishe njia yanapotokea majanga," anasema.

Changamoto nyingine kwa mujibu wa Ndesa ni kutokuwa na wataalamu wa kutosha wa uzimaji wa moto hali inayosababisha nguvu kazi kuwa ndogo pale majanga yanapotokea.

"Tukizidiwa sana inabidi tuombe nguvu kazi kutoka kwa wanakijiji ambao hawana elimu ya uzimaji moto kwa hivyo inabidi askari wawe nyuma yao kuhakikisha hawapati madhara."

Mara ya mwisho mlima huo kuwaka moto ilikuwa Oktoba, mwaka jana na kusababisha hekta 22.5 kuteketea, akisema juhudi za kuzima moto huo zilichukua takribani wiki mbili.

**WADAU WAONGEZA NGUVU**

Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Kaskazini, Lewis Nzali, ambao ndio wasimamizi wakuu wa mazingira kikanda, anasema huwa wanaongeza nguvu kwa KINAPA wakati wa kupambana na janga hilo.

"Huwa hatuwaachi, tunatuma nguvu kazi ikiwamo vifaa yakiwamo magari ya kuzimia moto, tunatoa vifaa vya kujikinga pamoja na wataalamu wa majanga ya moto ili kuongeza nguvu, na kama tukiona tumezidiwa tunakaa pamoja kama timu na kujadili nini kifanyike," anasema.

**Itaendelea kesho**

# Wizara Bara, Zanzibar sasa kushirikiana sekta ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA za Mifugo na Uvuvi, Kilimo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar zimekubaliana kufanya kazi pamoja katika utafiti wa magonjwa hatari ya mifugo, uzalishaji wa mifugo bora ya ng'ombe wa maziwa na huduma za mifugo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Katibu Mkuu kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof Elisante Ole Gabriel, alisema: "Tutashirikiana katika kuanzisha mashamba endelevu ya chakula cha ng'ombe, kudhibiti uingizaji wa bidhaa za ng'ombe nchini haswa maziwa yaliyosindikwa na kuku, nyama ya ngombe, kudhibiti magonjwa ya wanyama ya mpakani (TADs) na katika kutoa mafunzo maalum yanayohusiana na sekta ya mifugo."

Kwa muujibu wa Prof Ole Gabriel, timu maalum itaanzishwa Julai 15, mwaka huu na washiriki kutoka pande zote za Jamhuri ya Muungano ambao watapitia gharama za uzalishaji na usalama wa mazao ya mifugo na kushauri wizara juu ya nini kifanyike kutengeneza bidhaa za ndani kushinda masoko ya ushindani ndani ya mkoa na katika kiwango cha dunia.

"Tutashirikiana pia kuelimisha jamii ya wafanyabiashara, wasafirishaji na wadau wa tasnia ya maziwa kati ya bara na visiwani. Kuwaelimisha maafisa mipakani kwa kuwapa ujuzi kuhusu sheria na kanuni za sekta ya mifugo," a

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ya Zanzibar, Maryam Juma Sadala, alisema uhusiano huo utaenda mbali zaidi katika uzalishaji wa mifugo chotara kwa uzalishaji mkubwa wa maziwa.

"Kutakuwa na mipango ya kubadilishana wataalamu kutoka sehemu zote mbili kwenda kujifunza katika sehemu yoyote jinsi masuala ya mifugo yanavyoshughulikiwa. Lengo kuu la ushirikiano huu ni kujenga nguvu mpya ya ushindani kwenye sekta ya mifugo," alisema.

# Rais Samia aagiza usafirishaji korosho

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza korosho zinazolimwa katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi zisafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara.

Amesema serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika bandari hiyo kwa kuikarabati na kuipanua, hivyo kuna ulazima wa zao hilo kusafirishwa kupitia bandari hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa kikao na wadau wa korosho kilichofanyika Lindi, ilieleza kuwa Rais Samia amewaagiza viongozi wa bandari kupitia tozo zote zinazowakwaza wasafirishaji ili kuwavutia kuitumia bandari hiyo.

Waziri Mkuu alisema wakulima wakubali kupokea pembejeo kulingana na mahitaji yao, na watalipia kulingana na idadi ya mifuko waliyochukua na siyo Sh. 10 kwa kila kilo kama inavyelezwa.

Kadhalika, Waziri Mkuu alitoa wito kwa wakulima wa korosho kuwa na utaratibu wa kubangua korosho ili kupata faida zaidi badala ya kuziuza bila kuzibangua.

"Tungebangua wenyewe tungepata faida kubwa sana, wenye viwanda panueni viwanda vyenu na kukuza mitaji na wakulima wadogo endeleeni kubangua ili kuongeza thamani ya korosho zetu," alisema Majaliwa.

Alisema Serikali itaendelea kuwaunga mkono wadau wote wa korosho nchini katika kufanikisha mkakati huo ikiwamo kutengeneza mashine za ubanguaji kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO).

# 91 mbaroni kwa tuhuma za ujangili

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAMLAKA ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kanda ya Magharibi, imewakamata watu 91 wanaodaiwa kuwa ni majangili wakiwa na bunduki 24, risasi tisa na meno ya tembo manne wakiwa katika Hiifadhi ya Jamii katika Mkoa wa Tabora.

Kamanda wa Hifadhi ya Jamii, Bigilamungu Kagoma, alisema watuhumiwa hao walikamatwa baada ya kufanyika kwa msako maalum. Alitaja silaha zilizokamatwa ni SMG moja, Riffle tatu, Shotgun moja, na magobole 19. Alitaja makosa mengine yanayowakabili watuhumiwa hao ni uwindaji haramu wanyamapori, uharibifu wa mazingira na uvuvi haramu.

Kamanda Kagoma alisema doria zilizofanywa katika maeneo ya kati ya Pori la Akiba la Moyosi na eneo la Isawima zilifanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao.

Aidha, alisema Juni 3, mwaka huu bunduki moja aina ya gobole ilisalimishwa katika ofisi ya Kijiji cha Ugansa Wilaya ya Kaliua.

Alisema katika Pori la Akiba Ugalla watuhumiwa wawili walikamatwa, mmoja akiwa na gobole ambalo walikuwa wakitumia kuwindia.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

MALIPO YA KODI KWA AWAMU NA UWASILISHAJI RITANI KWA WAKATI

Ndugu Mlipakodi, unakumbushwa kulipa kodi ya mapato ya mwaka 2021 kadri ya awamu yako pamoja na kuwasilisha ritani ya kodi ya mapato ya mwaka 2020. Aidha, kama bado hujakadiriwa kodi ya mapato kwa mwaka 2021 tafadhali fika pia TRA ukadiriwe.

Wahi sasa ili kuepuka usumbufu usio wa lazima!.

TAHADHARI: Kuwa makini na matapeli wanaotumia vibaya jina la TRA au majina ya watumishi katika kipindi hiki, hivyo jiridhishe kila wakati.

Kumbuka: Ukiuza toa risiti. Ukinunua dai risiti

Kwa maelezoa zaidi, piga simu bure;
0800-750075 au 0800-780078
Barua pepe: huduma@tra.go.tz WhatsApp: 0744-233-333

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mbeya Kwanza, Geita Gold maandalizi Ligi Kuu ni sasa

**MBIO** za kuwania kupanda Ligi Kuu Bara hatua ya makundi kwa timu za Ligi Daraja la Kwanza, tayari zimehitimishwa kwa Mbeya Kwanza FC na Geita Gold FC kukata tiketi ya moja kwa moja baada ya kuibuka vinara katika wa Kundi A na B.

Timu hizo zimepanda moja kwa moja na zilizoshika nafasi ya pili Pamba FC na Transit Camp zikisubiri kujua wapinzani wao kutoka Ligi Kuu watakaokutana kwenye mechi ya mchujo kuwania nafasi mbili zilizosalia ili kukamilisha timu 16 zitakazoshiriki ligi hiyo msimu ujao.

Tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), limechezesha droo ya mechi hizo za mchujo, ambapo Pamba FC ya Mwanza itamenyana na timu itakayomaliza nafasi ya 13 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu huku Transit Camp ikimenyana na timu itakayomaliza nafasi ya 14 katika ligi hiyo.

Hivyo, huu ni wakati kwa Pamba na Transit Camp kuendelea kujifua kwa nguvu zikisubiri kujua wapinzani wao hao kuelekea mechi hizo, zitakazochezwa Julai 21, mwaka huu kabla ya kurudiana siku tatu baadaye.

Kwa upande wa Mbeya Kwanza na Geita Gold ambazo tayari zina tiketi ya kushiriki Ligi Kuu msimu ujao, zinapaswa kutambua haitakuwa ligi nyepesi, hasa kutokana na timu kupunguzwa kutoka 18 hadi 16, lakini pia ikiongezewa thamani baada ya Kampuni ya Azam Media kuongeza dau la udhamini wa kurusha matangazo.

Kwa ujumla, Nipashe tunatambua itakuwa ligi ngumu sana na yenye ushindani mkubwa kuanzia mwanzo hadi mwishoni mwa msimu, hivyo kama timu zilizopanda na zitakazopanda hazitajipanga mapema, kuna uwezekano wa kuwa za kwanza kurejea zilipotoka.

Katika kipindi hiki ligi ikiendelea, ni wakati wa makocha wa timu hizo kuifuatilia kwa makini na kutazama wachezaji wakuweza kuboresha vikosi vyao kwa ajili ya msimu ujao, badala ya kusubiri wale ambao watatemwa kutokana na viwango vyao kushuka.

Tunatoa tahadhari hiyo mapema kwa kuwa imekuwa kawaida kwa timu zinazopanda Ligi Kuu, kuvizia wachezaji wanaotemwa kutokana na kushuka viwango, ili kuimarisha vikosi vyao, jambo ambalo zinazifanya kushindwa kutoa ushindani mkubwa katika mbio za ubingwa, hivyo kubaki kwa 'farasa' watatu; Simba, Yanga na Azam, ambazo zimekuwa zikipokezana taji hilo kwa kipindi kirefu.

Nipashe tunatamani kuona timu zinazopanda Ligi Kuu zikija kutawala na kutoa changamoto kwa zilizopo ili ligi izidi kuwa ya kiushindani, hivyo ili hilo litimie, ni wakati kwao wa kuingia katika soko la usajili kwa kuchomoa wachezaji wenye uwezo mkubwa na si kusubiri wanaotemwa kutokana na kushuka viwango.


Lengo letu ni kuona Ligi Kuu Tanzania Bara ikitoka katika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika na kupanda juu zaidi, na hilo linawezekana tu kwa kila klabu kujipanga vema katika uwekezaji husussan kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya hali ya juu ili kwenda kutoa ushindani wa kweli.

Aidha, hatutaki kuona timu zilizopanda zikiwa za kwanza kupigania kujinasua katika msitari wa kushuka daraja mwishoni mwa msimu kama ilivyo sasa kwa Gwambina FC inayoshika nafasi ya pili kutoka mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu, hii ikiwa ni mara yao ya kwanza kushiriki ligi hiyo.

Katika hili, hakuna muujiza zaidi ya kila timu kujipanga ipasavyo kuelekea ligi hiyo, huku zikitambua kutegemea wachezaji waliozipandisha daraja pekee bila kuwaongezea wazoefu, kutaziweka katika wakati mgumu wa kuweza kutoa ushindani ligi hiyo itakapoanza msimu ujao.

Mfano halisi ni Ihefu FC, ambayo kama si kufanya maboresho kwa kusajili wazoefu katika usajili wa dirisha dogo, ilikuwa ikichungulia 'kaburi' la kushuka daraja, kabla kujinasua mzunguko wa pili ingawa bado nafasi ya 12 iliyopo kwa sasa haijawa salama sana kutokana na kutofautiana pointi moja tu na timu nne zinazoifuata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Inashangaza wabunge nao kuilalamikia TFF

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** ni siku ambayo yanasomwa mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ajili ya kupitishwa. Baada ya Waziri mwenye dhamana hiyo, Innocent Bashungwa, kumaliza, ikaanza michano ya Wabunge mbalimbali.

Baadhi walianza kulishutumu Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa madai ya kutoendesha soka vizuri na kusababisha lisiende mbele. Wapo waliosema inaliendesha kwa upendeleo. Wengine wakasema uendeshaji wao unafanya timu ya Taifa, Taifa Stars isifanye vema kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa.

Kuna wabunge ambao walidai wachezaji 10 wa kigeni kwenye klabu za Tanzania ni wengi, jambo ambalo linawafanya wachezaji wa Kitanzania washindwe kuonyesha vipaji vyao, hivyo timu ya taifa kukosa wachezaji bora.

Yupo hata aliyesema Tanzania ijitoe kwenye michuano yote ya kimataifa kwa miaka mitano ili ijipange. Ilikuwa ni baadhi tu ya michango ya wabunge, pamoja na mingi mizuri, lakini walionekana kujiondoa kwenye lawama ya kwa nini michezo yetu haisongi mbele nchini.

Labda kwa kujisahau, wabunge walionekana kuishambulia zaidi TFF kuliko vyama vingine vya michezo. Ilionekana kana kwamba TFF ndiyo wanasimamia michezo yote. Kwa ufupi michezo yote Tanzania iko hoi. Ngumi, riadha, netiboli na mingine mingi. Lakini TFF ndiyo iliyoshambuliwa sana.

Inawezekana TFF ikawa ina makosa, lakini soka la Tanzania lina matatizo makubwa ambayo yanaanzia mbali na shirikisho hilo linaweza kuchangia asilimia ndogo tu ya matatizo.

Nilidhani wabunge nao wangejiangalia kwa upande wao. Badala ya kuiangalia TFF, wangetoa michango ambayo ingesababisha michezo ya nchi hii kusonga mbele.

Badala ya kuishambulia TFF, wangeangalia kwanza jinsi nchi hii ilivyokuwa na upungufu wa viwanja vya wazi vya watoto kuchezea. Hilo lipo mikononi mwao.

Nchi ina uhaba wa sehemu za bustani kwa ajili ya kupumzikia kama ilivyokuwa zamani na viwanja vya wazi kwa ajili ya kuchezea watoto. Watoto wanapocheza ndipo wanaweza kuonyesha vipaji vyao na watu kuvuna wakiwa bado wadogo.

Zamani viwanja vilipokuwa vingi nchini, wachezaji wazuri walipatikana bila hata kuwa na shule za 'akademi' na walifanyia makubwa nchi hii.

Wabunge wangeangalia kwa nini shule nyingi kwa sasa hakuna viwanja vya michezo, badala yake yamejengwa madarasa? Hii haiwezi kusababisha vipaji vya soka nchini kupungua?

Leo hii Simba, Yanga na Azam ikitaka kusajili beki ni lazima iangalie nje ya nchi. Ni beki gani kwa sasa mzawa anayecheza Ligi Kuu nje ya timu hizi ambaye anaweza kwenda kuziba nafasi?

Wachezaji wengi wa Kitanzania wa sasa uwezo wao ni wa kawaida kwa sababu wamepambana wenyewe hadi kufikia hapo walipo na wala hakuna mfumo wowote rasmi uliofanya wawepo hapo.

Kwa hali hiyo haiwezekani ipatikane timu bora ya Taifa, Taifa Stars. Badala yake tumejikita kutaka kupunguza wachezaji wa kigeni, tena kwenye timu tatu tu za Simba, Yanga na Azam, kana kwamba timu hizi ndiyo vitalu vya Stars.

Wakati Watanzania tunataka kufanya hivyo, wenzetu nchini mwao wanawawekea mazingira bora wachezaji wao na kusambaa kote duniani, hivyo wakiita kikosi chao cha taifa, kinatoka pembe zote za dunia, huku Tanzania tukitaka eti watoke Simba, Yanga na Azam.

Klabu hizi lengo lake ni kushinda ubingwa na mataji yote, pamoja na kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa, hivyo haiwezekani kuwapangia wachezaji.

Simba hii ambayo imefika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ingekuwa na wachezaji wa Kitanzania, sidhani hata kama ingeitoa Plateau United ya Nigeria kwenye mechi ya awali.

Wabunge walitakiwa waisimamie serikali, badala ya kujitoa kwenye michuano, iruhusu uraia pacha hata kwa wanamichezo tu ili nchi ipate wachezaji wenye uraia wa nchi mbili kwa ajili ya kuisaidia Taifa Stars kwenye soka na hata michezo mingine.

Kwa sasa nchi kama Comoro, Madagascar, Cape Verde zimepiga hatua kisoka kwa sababu hiyo. Zina wachezaji wa nchini mwao wenye asili ya Kireno na Kifaransa wanaocheza nje kwenye madaraja ya chini, wanaporudi Afrika wanawasaidia sana.

Haya ndiyo baadhi ya mambo ambayo wabunge wetu walisahau kuyazungumza na wanapaswa kuyazungumza sasa ambayo yatakuwa na afya kwenye soka letu na si kuishambulia TFF.

**HABARI KITAIFA**

# Vikwazo vya utekelezaji miradi ya ubia vyatajwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imesema licha ya nia njema iliyonayo ya kuhusisha sekta binafsi kutekeleza baadhi ya miradi mikubwa ya kufua umeme kama wa Kampuni ya IPTL, Kampuni ya Maji ya City Water na Kampuni ya Uendeshaji wa Reli ya RITES ya India, miradi hiyo haikufanikiwa kutokana na kasoro mbalimbali.

Miongoni mwa mambo yanayotajwa kusababisha hali hiyo ni pamoja na kukosekana kwa mazingira wezeshi yenye kuelekeza taratibu za kufuata katika kufanya maandalizi kabla ya kuingia mikataba ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuleta tija na manufaa kwa taifa.

Hayo yamo katika hotuba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, aliyoisoma jijini Arusha, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini.

"Nakaribisha wadau wa sekta binafsi, sababu utaratibu wa PPP nchini ulianza rasmi kama azma ya serikali kuimarisha mazingira wezeshi ya kuishirikisha sekta binafsi katika kuleta maendeleo kama mhimili mkuu wa uchumi.

"Moja ya mipango ya serikali ya kutekeleza azma hii, ilikuwa kuandaa Sera ya PPP ya mwaka 2008, Sheria ya PPP ya mwaka 2010, Sura ya 103 na Kanuni zake."

Alisema uwekezaji huo, utasaidia kukuza uchumi wa nchi na kila mmoja kupata maendeleo.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, serikali ilihusisha sekta binafsi kutekeleza baadhi ya miradi kama ya IPTL, City Water na RITES-India, hata hivyo, haikufanikiwa kutokana na matatizo mbalimbali.

"Tunaendelea kualika wadau wa sekta binafsi kushirikiana kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma, na wao kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi, uchukuzi, elimu na viwanda ili kuinua uchumi nchini.

Maeneo mengine ya uwekezaji ni hospitali, bandari, michezo, biashara na uchukuzi. Hadi sasa jumla ya miradi 41 imeandaliwa na kufanyiwa uchambuzi, kati ya hiyo 40 imeandaliwa na mamlaka za serikali na mradi mmoja, umeandaliwa na mwekezaji kutoka sekta binafsi."

"Kati ya miradi hiyo, mitano ipo katika hatua za kuwatafuta wabia na mingine iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi," alisema Katibu Mkuu Tutuba.

Alisema jitihada hizo zitachangia kujenga uchumi shindani na wa viwanda kwa maendeleo ya watu ifikapo mwaka 2025/26 na serikali kupata ubunifu, utaalamu na teknolojia kutoka sekta binafsi.

Naye, Kamishna wa PPP, Dk. John Mboya, alisema utaratibu wa ubia ni njia muhimu na vyanzo mbadala vya mapato vya kugharamia miradi ya maendeleo.

Alisema serikali imeanisha miradi ya PPP inayotekelezwa ili kuchangia kikamilifu kugharamia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026, ambao umeweka kipaumbele kutumia vyanzo bunifu ikiwamo PPP.

"Hadi mwezi Mei 2021 jumla ya miradi 41 ipo katika hatua mbalimbali za maandalizi na thamani yake katika hatua zote imekadiriwa ni zaidi ya Sh. trilioni 3.042. Kwa mujinu wa Dk. Mboya, ili kufikia azma ya kutekeleza Programu ya PPP na kwa kasi inayotakiwa, elimu imetolewa na kabla ya mwaka huu wa fedha, zaidi ya wadau 829 wameshapatiwa elimu hiyo, huku mchakato huo ukiendelea.

# Kero Mto Msimbazi Dar kumalizwa

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameahidi kumaliza kero ya mafuriko mto Msimbazi ifikapo mwakani.

Ummy aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Aliuagiza uongozi wa DMDP kuhakikisha unatafuta mwarobaini wa kudumu wa mto Msimbazi ili wananchi wafanye shughuli zao kama ilivyokuwa awali.

"Kwa mto Msimbazi tunataka kujenga daraja likiwa na kingo zake, kaeni chini mtafakari ikiwezekana ifikapo Desemba 2022 tusahau mafuriko ya Dar es Salaam," alisema Ummy.

Aidha, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya malipo ya fidia ya wananchi waliopisha ujenzi wa mto Ng'ombe na tayari zimehamishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kinondoni.

Alisema jumla ya wananchi 423 wanatakiwa kupatiwa fedha hizo na baada ya kufanya tathmini wamebaini wananchi 375 wanapaswa kulipwa.

Ummy pia aliagiza katika awamu ya pili ya mradi wahakikishe wanazingatia haki na usawa katika ugawaji wa rasilimali kwa kila Manispaa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliahidi kufuatilia miradi yote inayotekelezwa ili kujiridhisha kama imekidhi vigezo.

"Nitaipitia miradi yote ambayo tayari nitapita kujiridhisha kama imekidhi viwango na nitafanya kazi hiyo vizuri," alisema Makalla.

Kuhusu fidia ya wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi mto Ng'ombe, alisema fedha zimefika na zipo kwa Mkurugenzi, lakini baadhi wa wananchi wametoa malalamiko kuwa fedha wanazotakiwa kulipwa ni ndogo na tofauti na tathmini ilivyofanyika na kwamba waliamua kujiridhisha kabla ya malipo.

Makalla alisema serikali haipaswi kulaumiwa kwa kuwa fedha zipo na wananchi watalipwa huku kazi ya uhakiki ikiendelea kufanyika.

Msimamizi wa miradi inayosimamiwa na Benki ya Dunia, Humphrey Kanyenye, alisema mradi wa DMDP umegharimu Sh. milioni 690 na utekelezaji wake ulianza Juni mwaka 2015 na unatarajiwa kuisha mwakani, utekelezaji wake umefika asilimia 85.

Alisema mradi huo unatekelezwa baada ya sensa iliyofanyika na kubaini mwaka 2030, Dar es Salaam inakadiriwa kuwa na watu milioni 10.

**Kuhusu fidia ya wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi mto Ng'ombe, alisema fedha zimefika na zipo kwa Mkurugenzi, lakini baadhi wa wananchi wametoa malalamiko kuwa fedha wanazotakiwa kulipwa ni ndogo na tofauti na tathmini ilivyofanyika na kwamba waliamua kujiridhisha kabla ya malipo.**






Wafanyakazi wa mgodi wa Barrick- North Mara wakishiriki zoezi la kupanda miti kwenye eneo la mgodi katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanahisa NMB kulipwa gawio la bil. 68.5/-

**Na Elizabeth Zaya**

WANAHISA wa Benki ya NMB wanatarajiwa kulipwa gawio la Sh. bilioni 68.5, Juni 16, mwaka huu ambalo limetokana na faida ya mwaka 2020, huku wanahisa wakubwa kampuni ya Arise ikitarajiwa kulipwa Sh. bilioni 23.9 na serikali Sh. bilioni 21.8.

Matokeo ya wanahisa kulipwa gawio hilo ni baada ya benki hiyo kupata faidamwaka jana ikiwamo kuvuka lengo la faida yake.

"Kiasi cha gawio kilichotengwa mwaka 2020 ni sawa na ongezeko la asilimia 43 kutoka Sh. bilioni 48 zilizolipwa mwaka 2019. Huu ni mwaka wa tatu mfululizo kwa benki kuongeza gawio kwa wanahisa wake," alisema Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna.

"Ongezeko la gawio linalolipwa linadhihirisha ufanisi mzuri wa utekelezaji wa mikakati ya benki kwa mwaka 2020 pamoja na mtaji imara wa Benki ya NMB."

Zaipuna alisema mafanikio mengine ambayo benki hiyo ilipata mwaka jana ni pamoja kuushusha uwiano wa mikopo chechefu hadi asilimia tano. Zaipuna alisema benki hiyo itaendelea kujiimarisha katika misingi imara ili kuhakikisha biashara yake inakuwa endelevu na kujikita katika kutoa huduma bora zaidi, za kibunifu na zinazokidhi matarajio ya wateja na wadau wake wote.

Alisema wataendelea kusaidia kufanikisha kuboresha maisha na uchumi wa Tanzania katika utekelezaji wa ajenda yake ya maendeleo kupitia huduma zenye ubora wa kimataifa na faida kwa wawekezaji.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Dk. Edwin Mhede, alisema gawio hilo linadhihirisha utendaji kazi mzuri na unaoongeza thamani.

"Gawio lililoidhinishwa linadhihirisha utendaji mzuri unaoongeza thamani kwa wadau wetu. Tunaahidi kuendeleza juhudi hizi kuongeza faida kwa wanahisa wetu na jamii tunayoihudumia. Tutaendelea kuhakikisha tunatimiza ndoto na malengo yetu na wanahisa," alisema Dk. Mhede.

"Pamoja na athari za janga la Covid-19, faida ya mwaka 2020 iliongezeka kwa asilimia 45 kulinganisha na mwaka uliotangulia, hivyo kuweka rekodi ya faida kubwa kuwahi kutengenezwa."

Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Juma Kimori, alisema mwenendo huo unaeleza jinsi wanavyoendelea vyema kutekeleza mpango mkakati waliyojiwekea.




# Tanzania yapeleka China tani 120 za soya

**Na Mwadishi wetu**

TANZANIA imefanikiwa kusafirisha zaidi ya tani 120.2 za maharagwe ya soya kwenda China, baada ya kufikia makubaliano ya kusafirisha mazao hayo kati ya nchi hizo.

Makubaliano hayo yalifikiwa mwaka jana, baada ya kuona mahitaji ya nchi hiyo kuwa ni zaidi ya tani milioni 103, huku zaidi ya tani milioni 15 zikizalishwa nchini humo na milioni 88 zinategemewa kutoka nchi nyingine ikiwamo Tanzania.

Soya ni moja ya mazao yanayohitajika kwa ajili ya protini na mafuta, huku Tanzania ikiwa ni moja ya nchi inayopeleka zao hilo nchini humo.

Naibu Mkurugenzi wa kitengo cha ukaguzi Kituo cha Forodha cha Huangdao China, Kong Farming, alisema anafuatilia kwa karibu nafaka zinazoingia nchini humo, na kwamba wanawasaidia wajasiriamali kupunguza gharama, na kuhakikisha ubora wa kila bidhaa.

Alisema maharagwe ya soya kutoka Tanzania yamebainika kuwa na ubora unaotakiwa, baada ya ukaguzi wa kina unaofanywa na kituo cha forodha nchini humo.

Februari mwaka huu, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alilileza Bunge kuwa, Tanzania ni kati ya nchi 12 zilizoruhusiwa kupeleka soya nchini humo.

Aidha, alisema licha ya fursa hiyo uzalishaji ni mdogo kulingana na mahitaji ya China na bara la Asia kwa ujumla, na kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa hiyo.

China ni mnunuzi mkubwa wa soya duniani na imefungua milango kwa Tanzania, kwa mujibu wa takwimu zao hilo, uzalishaji ni zaidi ya tani 1,000.

# Wanasayansi chipukizi kuibuliwa mikoa 25

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Young Scientists Tanzania (YST), inatarajia kufanya maonyesho ya kuibua wanasayansi chipukizi katika mikoa 25 ya Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gozibert Kamugisha, alisema miaka yote walikuwa wanayafanyia katika mkoa wa Dar es Salaam pekee, lakini mwaka huu wameamua kupanua wigo.

Dk. Kamugisha alisema maonyesho hayo yanashirikisha wanasayansi chipukizi kutoka katika shule za sekondari, na kwamba wamepokea maombi 579 ya kazi za kisayansi na ugunduzi yaliyowasilishwa na wanafunzi hao.

"Kutokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wanafunzi katika tafiti za kisayansi na ugunduzi, YST imefanya uamuzi wa kufanya maonyesho ya wanasayansi chipukizi katika mikoa 25 mwaka huu, uamuzi huu unatoa fursa kubwa kwa shule na wanafunzi wengi zaidi kushiriki katika programu hii ya wanasayansi," alisema Dk. Kamugisha.

"Kuanzishwa kwa kwa maonyesho ya chipukizi kwenye mikoa kutatoa fursa kwa mamlaka za mikoa hasa TAMISEMI, kushirikiana na YST katika ustawi wa programu hii na katika mwaka huu wa kwanza kuanzisha maonyesho ya wanasayansi chipukizi ngazi ya mikoa, yatajumuisha kazi za ugunduzi zisizopungua 12."

Dk. Kamugisha alisema kazi za kisayansi na ugunduzi zaidi ya 300 zitaonyeshwa katika maonyesho hayo ya wanasayansi chipukizi katika mikoa hiyo.

Alisema kazi za kisayansi na ugunduzi zenye ubora zisizopungua sita zitachaguliwa kutoka katika maonyesho hayo ya kila mkoa, na zitashindanishwa miongoni mwa kazi 150 katika maonyesho ya kitaifa yatakayofanyika kwa njia ya mtandao Oktoba, mwaka huu.

# TANGAZO

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

## "EXIM AT WORK, TODAY, FOR TOMORROW"

EXIM AT WORK TODAY | FOR TOMORROW

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA ZILIZOKAGULIWA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 & ya 8 ya kanuni za mabenki na taasisi za fedha (Uoneshaji) ya mwaka 2014

**Fedha za Wanahisa @ TZS Bilioni 179**

**Jumla ya Mali @ TZS Trilioni 1.96**

**Amana za Wateja @ TZS Trilioni 1.44**

**Mikopo Halisi @ TZS Trilioni 1**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2020 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2019 | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2020 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2019 |
|---|---|---|---|---|
| **A MALI** | | | | |
| 1 Fedha Taslimu | 60,994 | 42,243 | 51,101 | 24,393 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 246,331 | 136,401 | 67,151 | 67,683 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 324,196 | 244,827 | 313,821 | 241,033 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 34,595 | 70,955 | 21,935 | 31,796 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 2,357 | 3,692 | 1,394 | 1,953 |
| 6 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 39,340 | 158,631 | 10,504 | 111,051 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 29,301 | 30,583 | 5,122 | 7,797 |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 1,095,304 | 953,374 | 699,928 | 708,745 |
| 12 Mali nyingine | 38,470 | 44,348 | 32,984 | 38,808 |
| 13 Uwekezaji katika Hisa | 2,447 | 2,529 | 35,310 | 36,253 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 77,324 | 81,414 | 51,318 | 60,090 |
| 16 Mali isiyo ya sasa yanayotumiwa | 13,751 | 16,907 | 12,905 | 15,949 |
| **17 JUMLA YA MALI** | **1,964,410** | **1,785,904** | **1,303,473** | **1,345,551** |
| **B DHIMA** | | | | |
| 18 Amana za Benki na Taasisi za Fedha | 135,586 | 98,993 | 212,518 | 273,720 |
| 19 Amana za Wateja | 1,441,605 | 1,298,177 | 755,488 | 721,308 |
| 20 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 25,445 | 8,486 | 23,202 | 6,852 |
| 21 Amana Maalumu | - | - | - | - |
| 22 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 282 | 282 | 282 | 282 |
| 23 Hundi na Hawala za Kibenk Zilitolewa | 2,111 | 2,843 | 1,492 | 1,576 |
| 24 Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,989 | 4,941 | 3,988 | 4,160 |
| 25 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya benki | - | - | - | - |
| 26 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 27 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 6,833 | 9,365 | 6,285 | 8,851 |
| 28 Dhima Nyingine | 58,576 | 60,468 | 34,835 | 42,498 |
| 29 Madeni | 110,460 | 144,220 | 110,460 | 144,220 |
| **30 JUMLA YA DHIMA** | **1,785,887** | **1,627,775** | **1,148,550** | **1,203,467** |
| **31 MALI/(DHIMA) HALISI (17 kutoa 30)** | **178,523** | **158,129** | **154,923** | **142,084** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 32 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 12,900 | 12,900 | 12,900 | 12,900 |
| 33 Akiba ya Mtaji | 31,253 | 44,416 | 19,088 | 37,996 |
| 34 Mapato Yaliyobakizwa | 108,217 | 103,873 | 110,600 | 108,957 |
| 35 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 15,892 | -14,993 | 12,335 | -17,769 |
| 36 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - | - | - |
| 37 Stahiki ya Wenyehisa Chache | 10,261 | 11,933 | | |
| **38 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **178,523** | **158,129** | **154,923** | **142,084** |
| 39 Dhima Zisizo Dhahiri | 222,717 | 203,516 | 160,425 | 141,508 |
| 40 Mikopo Chechefu | 144,858 | 199,022 | 122,508 | 169,393 |
| 41 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 54,364 | 78,457 | 43,093 | 57,825 |
| 42 Mali Nyingine Chechefu | 2,799 | 2,914 | 2,799 | 2,914 |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.09% | 8.85% | 11.89% | 10.56% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 12.75% | 22.66% | 16.79% | 22.06% |
| Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76.91% | 75.56% | 79.32% | 77.16% |
| Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.76% | 53.38% | 53.70% | 52.67% |
| Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77.64% | 81.80% | 83.36% | 84.48% |
| Ongezeko la Amana | 12.88% | 11.49% | -2.72% | 7.47% |
| Ongezeko la Mali | 10.00% | 14.16% | -3.13% | 11.21% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI MWAKA WA SASA 31.12.2020 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2019 | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2020 | KAMPUNI MWAKA ULIOPITA 31.12.2019 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 141,034 | 130,794 | 107,134 | 102,552 |
| 2 Gharama za Riba | (41,810) | (38,997) | (36,592) | (35,627) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **99,224** | **91,797** | **70,542** | **66,925** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 74 | (39,994) | 3,563 | (30,352) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **59,658** | **57,201** | **36,823** | **34,442** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 16,962 | 13,807 | 10,731 | 8,757 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 33,611 | 35,817 | 17,154 | 20,226 |
| 6.3 Gawio | 40 | 21 | 3,014 | 21 |
| 6.4 Mapato Mengine | 9,045 | 7,556 | 5,924 | 5,438 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(129,163)** | **(117,382)** | **(88,570)** | **(85,541)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (55,966) | (53,058) | (36,481) | (35,578) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (140) | (174) | (140) | (161) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (73,057) | (64,150) | (51,949) | (49,802) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **29,793** | **(8,378)** | **22,358** | **(14,526)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (13,901) | (6,615) | (10,023) | (3,243) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **15,892** | **(14,993)** | **12,335** | **(17,769)** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 962 | 1,001 | 619 | 688 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 1,232 | (1,162) | 956 | (1,377) |
| 13 Idadi ya Matawi | 45 | 48 | 30 | 33 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1% | -1% | 1% | -1% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9% | -10% | 8% | -13% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 75% | 83% | 73% | 85% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7% | 8% | 7% | 6% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020
z(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2020 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2019 | KAMPUNI MWAKA WA SASA 31.12.2020 | KUNDI MWAKA ULIOPITA 31.12.2019 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 29,793 | (8,378) | 22,358 | (14,526) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| -Hasara Katika Mali | 28,071 | 68,148 | 17,127 | 50,449 |
| -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (150,257) | (113,181) | 7,634 | (78,497) |
| -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 125 | (41) | 186 | (7) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 180,021 | 144,043 | (27,022) | 69,165 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 41,840 | 18,947 | 24,571 | 24,566 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (793) | 1,012 | (1,668) | 3,280 |
| -Non-current assets held for sale | - | - | - | - |
| -Kodi Iliyolipwa | (9,874) | (6,570) | (8,087) | (4,731) |
| -Mengineyo (bainisha) | (76,590) | (9,727) | (68,463) | (21,028) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **42,335** | **94,253** | **(33,364)** | **28,671** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 40 | 21 | 3,014 | 21 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (15,525) | (11,493) | (4,264) | (5,572) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 804 | 380 | 562 | 7 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (Uwekazaji katika hisa) | - | (4,050) | - | (4,050) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(14,681)** | **(15,142)** | **(688)** | **(9,594)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (43,111) | (26,932) | (43,111) | (27,069) |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | 62,159 | - | 62,159 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 2,863 | - | (4,053) |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (10,785) | (12,570) | (5,809) | (7,049) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(53,896)** | **25,520** | **(48,920)** | **23,988** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (26,242) | 104,631 | (82,972) | 50,987 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka 336,811 | 205,184 | 187,570 | 136,583 | |
| Mabadiliko ya Miamala ya Fedha za Kigeni na Ziada ya Fedha | (13,185) | 26,996 | 884 | 7,922 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | **297,384** | **336,811** | **105,482** | **187,570** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2020 Kiasi kwa shilingi milioni)

| KAMPUNI | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **12,900** | **-** | **91,188** | **37,372** | **-** | **624** | **142,084** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 12,335 | - | - | - | 12,335 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 504 | 504 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 19,412 | (19,412) | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2020** | **12,900** | **-** | **122,935** | **17,960** | **-** | **1,128** | **154,923** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **12,900** | **-** | **135,452** | **10,877** | **-** | **-** | **159,229** |
| Mabadiliko ya mwanzo ya IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Marekebisho mengine | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **12,900** | **-** | **135,452** | **10,877** | **-** | **-** | **159,229** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (17,769) | - | - | - | (17,769) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 624 | 624 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | 6,402 | (6,402) | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (32,897) | 32,897 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **12,900** | **-** | **91,188** | **37,372** | **-** | **624** | **142,084** |
| **KUNDI** | | | | | | | |
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **12,900** | **-** | **88,880** | **40,042** | **-** | **16,307** | **158,129** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 17,570 | - | - | (1,678) | 15,892 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 4,502 | 4,502 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 20,929 | (20,929) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (3,270) | 3,270 | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2020** | **12,900** | **-** | **124,109** | **22,383** | **-** | **19,131** | **178,523** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **12,900** | **-** | **129,395** | **13,341** | **-** | **10,814** | **166,450** |
| Mabadiliko ya mwanzo ya IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Marekebisho mengine | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio jipya la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **12,900** | **-** | **129,395** | **13,341** | **-** | **10,814** | **166,450** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (13,814) | - | - | (1,179) | (14,993) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 3,809 | 3,809 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | 2,863 | 2,863 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 6,196 | (6,196) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (32,897) | 32,897 | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2019** | **12,900** | **-** | **88,880** | **40,042** | **-** | **16,307** | **158,129** |

Dondoo za hapo juu zimetokana na mahesabu ya Benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2020 ambazo zimetayarishwa kwa kuzingatia kanuni za kihasibu za taarifa za kiwango cha kimataifa (IFRS). Taarifa za mahesabu haya zilikaguliwa na Deloitte & Touche "Certified Public Accountant" na kupatiwa hati safi.

Taarifa za mahesabu hapo juu ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi tarehe 01 Juni 2021 na kutiwa sahihi na wajumbe wafuatao hapa chini.

| JINA NA CHEO | SAINI | TAREHE |
|---|---|---|
| Balozi Juma Mwapachu<br>**MWENYEKITI WA BODI** | ...................................... | 01.06.2021 |
| KALPESH MEHTA<br>**MKURUGENZI** | ...................................... | 01.06.2021 |

Kwa maelezo zaidi tupigie 0800780111 au tembelea www.eximbank.co.tz

EXIM BANK
Innovation is life




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija, akimkabidhi Afisa Mwandamizi wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Lameck Charles (kushoto), tuzo maalum baada ya benki hiyo kuibuka kinara wa kutunza na kuhifadhi mazingira miongoni mwa taasisi za kifedha jijini Dar es Salaam, katika serehe za kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kwenye viwanja vya Mnazimmoja mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaozuia watoto kwenda shule watozwa faini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI katika Manispaa ya Shinyanga imeanza kuwatoza faini ya mifuko ya saruji wazazi ambao wanawazuia watoto wao wa kike kwenda shule.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, Wilson Mwakaluba, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema katika suala la mapambano ya kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, wameona ni vyema kuanza kuwawajibisha wazazi wanaokatisha masomo ya watoto wao wa kike kwa kuwatoza mifuko ya saruji. Alisema baadhi ya wazazi ni chanzo cha kukwamisha watoto wao wasipate elimu, badala yake kutaka wabaki nyumbani ili wawaozeshe.

"Mfano sasa hivi katika Shule ya Msingi Galamba, kuna mwanafunzi ameshapewa ujauzito na ametoroshwa na mama yake na hajulikani alipo...na mwaka huu tuna jumla ya mimba tano, sekondari mimba nne na moja shule ya msingi," alisema Mwakaluba.

Aidha, alisema baada ya kuanza kutoza wazazi mifuko ya saruji kwa mwezi mmoja, utoro kwa wanafunzi umepungua shuleni.

Naye Diwani wa Kolandoto, Mussa Andrew, alisema wamekuwa wakiendesha mikutano ya hadhara kwa kushirikiana na maofisa maendeleo na ustawi kwa lengo la kueleza wanaume kuacha kuwalaghai wanafunzi badala yake wawaache watimize ndoto zao.

Baadhi ya wazazi walisema suala hilo la kuwajibishwa kwa kutozwa mifuko ya saruji ni jema, kwa kuwa litasaidia kutokomeza mimba na ndoa za utotoni.

# Wajasiriamali wa maziwa waona faida ubora bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI kubwa ya wafanyabiashara na wajasiriamali walioshiriki Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa yaliyofanyika mkoani Tanga kuanzia Mei 31 hadi Juni 4, mwaka huu wamebainika kuthibitisha ubora wa maziwa.

Hiyo inadhihirisha kuongezeka kwa mwamko wa Watanzania kujua faida za kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki, kwenye maonyesho hayo, wafanyabiashara hao walisema kwa sasa wanaona waziwazi faida za kuthibitisha ubora wa maziwa yao, kwa sababu hawakabiliani na vikwazo vya kibiashara kama ilivyokuwa awali.

Endrew Swai, alisema kabla ya kuthibitisha ubora wa maziwa yake Shirika la Viwango Tanzania (TBS) mara kwa mara, watu walikataa kuyanunua kwa sababu walikuwa hawaoni alama ya ubora ya TBS.

"Lakini tangu tumethibitisha ubora tumeweza kuingia kwenye soko hata la Jumuiya ya Afrika Mashariki bila vikwazo, lakini mwanzo ilikuwa vigumu," alisema Swai.

Naye Jacob Msukuma, kutoka mkoani Mwanza alisema kuanzishwa kwa ofisi za kanda za TBS imewapa urahisi wao kuthibitisha ubora wa maziwa yao, kwa sababu wanapata msaada wa karibu kutoka kwa maofisa wa shirika hilo.

Afisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alisema: "Cha kufurahisha kwenye maonesho haya asilimia kubwa ya watu walioshiriki wamethibitisha ubora wa maziwa yao TBS.

Ambao hawajathibitisha ni wachache na tulipowaulizwa walisema wapo kwenye mchakato, lakini pia tumewaelekeza taratibu za kufuata ili kuthibitisha ubora bidhaa zao waweze kupata alama ya TBS."

Mayugu alisema kupitia maonyesho hayo walitoa elimu kwa wadau hao kuhusiana na umuhimu na faida za kuthibitisha ubora wa bidhaa zao, hatua ambayo itawasaidia kuondokana na vikwazo vya kibiashara, kupanua wigo wa soko la maziwa yao na kujenga imani kwa wananchi kuwa maziwa yao ni salama kwa afya ya walaji.

# Tigo yakabidhiwa miche ya miti 7,000

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania, imepokea miche 7,000 ya miti kutoka Helios Towers Tanzania, ikiwa ni mchango wa upandaji miti wa kampeni ya Tigo Green For Kili.

Kampeni hiyo ni kwa ajili ya kupanda miti kwenye eneo la Mlima Kilimanjaro ya Tigo Green For Kili ambayo mikakati yake ni kupanda miti 28,000, maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Kampeni hiyo ilizinduliwa Februari, mwaka huu na Tigo imeshapokea miche kutoka kwa wadau mbalimbali.

Miche 7,000 ya miti imetolewa na Helios Towers Tanzania, tayari kampeni hiyo imeshakusanya mchango wa miche 31,446 kutoka Tigo na wadau mbalimbali kwa ajili ya kampeni ya Tigo Green For Kili.

Akizungumza wakati wa makabidhiano katika Wilaya ya Hai, Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Daniel Mainoya, alisema: "Ni imani yetu kuwa miti hii itasaidia kurejesha sehemu ya theluji kwenye Mlima Kilimanjaro ambayo tumeshuhudia ikipungua kwa miaka minne iliyopita kwa sababu ya ongezeko la joto duniani.

"Ninawashukuru Helios Towers Tanzania kwa kuchangia miche ya miti 7,000 katika kampeni hii. Ninawaomba wadau wengine wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuhakikisha tunafikia malengo kwani tunaendelea kupokea miche," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Helios Towers Tanzania, Ramsey Koola, alisema kampuni hiyo ina jukumu muhimu katika kuwezesha na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo mbalimbali.

Alisema mikakati yao ni kuhakikisha kukuza na kuendeleza miundombinu ili kupunguza mzigo wa mazingira kwa jamii.

# Wafanyakazi majumbani wafundwa kujua haki zao

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WANAWAKE wanaofanya kazi za ndani wamepatiwa mafunzo ili kutambua aina za ukatili katika sehemu zao za kazi pamoja na kujua umuhimu wa kupima afya zao.

Kadhalika, wamejengewa uwezo wa namna ya kujiepusha na ukatili mbalimbali wanaokutana nao katika maeneo yao pamoja na kujua wajibu na haki zao.

Mafunzo hayo yalitolewa jana jijini Mwanza na Ofisa mradi wa usawa kwa wanawake wafanyakazi wa majumbani kutoka Shirika la WoteSawa.

Wafanyakazi hao 30 kutoka Mtaa wa Nyamagana Mashariki, Kata ya Nyamagana jijini Mwanza, walipatiwa mafunzo hayo ya siku mbili ili kuwajengea uwezo kukabiliana na matatizo mbalimbali wanayokutana nayo sehemu zao za kazi.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka shirika la WoteSawa, Demitila Faustine, alisema wanawake hao wanakutana na mambo mengi, na kwamba elimu hiyo itawasaidia kujua haki zao.

Aidha, alisema mafunzo hayo pia yatawasaidia kujua afya zao kwa sababu hivi sasa kuna wimbi la kansa ya shingo ya uzazi ambalo huwakumba wanawake.

Maeneo mengine waliyowafundisha ni pamoja na kukabiliana na ukatili wa kingono wanaofanyiwa wanawake hao majumbani wanapofanyia kazi.

Domitila alisema wanawake hao wanapaswa kupatiwa elimu sahihi ili kuhamasika kupima magonjwa mbalimbali ikiwamo Ukimwi kwa sababu wanawake wengi wanafanyiwa ukatili wa kingono na waajiri wao.

Nipashe Spotika



WACHEZAJI 10 BORA MABINGWA ULAYA 2020/21 UK. 12-13



# STRAIKA WA5 WANAOWEZA KUSHANGAZA EURO 2020

GERARD MORENO

**LONDON,** England

MENGI yanatarajiwa kwenye michuano ya Euro 2020, ambayo itaanza kutimua vumbi Jumamosi ijayo, huku bingwa mtetezi Ureno akiwa kwenye harakati za kutetea taji lake. Kutakuwa na timu kubwa na zenye historia kubwa kwenye soka la dunia.

Italia itafungua pazia la michuano hiyo kwa kucheza na Uturuki pale kwenye dimba la Olimpico.

Makala haya inawaangalia mastraika watano ambao wanaweza kushangaza kwenye Euro 2020, twende sasa...

**#5. ANTE REBIC | CROATIA**

Ni straika wa AC Milan na alikuwa shujaa wa Croatia wakati wakitinga fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2018. Ante Rebic anaweza kuthibitisha ubora wake kwenye michuano ya Euro akiwa na Croatia ambayo inapenda kucheza kwa staiili ya mashambulizi ya kushitukiza.

Rebic alifurahia msimu mzuri wa 2020-21akiwa na 'Rossoneri' baada ya kusajiliwa kwa mkataba wa kudumu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, pia alikuwa na msimu wa kuvutia wakati akicheza kwa mkopo AC Milan na ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu.

Katika mechi 33, alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu, Rebic alihusika katika mabao 17 (akitoa pasi za mwisho sita). Rebic ana ubora wa aina yake katika kufunga. Nyota huyo alicheza mechi 19 akiwa nafasi ya wiga wa kushoto msimu huu, mara nyingi ni pale ambapo Zlatan Ibrahimovic alikuwapo.

**#4. BURAK YILMAZ | UTURUKI**

Burak Yilmaz amekuwa mmoja wa wachezaji wenye kiwango bora kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, msimu huu, akitoa mchango mkubwa kwa Lille waliobeba taji la Ligi Kuu.

Uturuki ni kama farasi mweusi kwenye michuano ya Euro 2020, na straika wao huyo nyota ana tumainiwa kufanya makubwa. Katika mechi 33, alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu, Yilmaz amefunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho tano.

Alikuwa mfungaji bora zaidi wa Lille kwenye Ligue 1 msimu huu. Yilmaz anatarajiwa kuwa patina wa Hakan Calhanoglu kwenye michuano hiyo.

**#3. ARTEM DZYUBA |URUSI**

Kama ilivyo kwa Yilmaz, Dzyuba ni mmoja wa mastraika wanaotarajiwa kuchomoza kwenye Euro 2020. Ni nyota wa kikosi cha Urusi ambaye ana uzoefu wa kutosha kuanza kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 ambapo nchi yake iliandaa. Dzyuba amejipambanua mwenywe kwenye soka la Urusi.

Mabao yake dhidi ya Hispania, Misri na Saudi Arabia, pamoja na pasi za mwisho za kutosha zinamfanya kuwa na wakati mzuri. Alikuwa kwenye kiwango bora akiwa na Zenit St. Petersburg na amekuwa mchezaji muhimu kwa timu yake.

Katika mechi 34 kwenye mashindano yote msimu huu, amehusika katika mabao 29 (mabao 22 na pasi za mwisho saba). Dzyuba amefunga mabao 13 kwenye mechi za kimataifa tangu Kombe la Dunia mwaka 2018. Urusi ilitinga nusu fainali ya michuano ya Euro mwaka 2008.

**#2. DONYELL MALEN | UHOLANZI**

Donyell Malen amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu akiwa ndiye mfungaji tegemezi wa PSV Eindhoven. Mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal alihamia Uholanzi mwaka 2017 wakati wa kipindi cha dirisha la majira ya joto.

Malen kwa kipindi cha misimu miwili iliyopita klabuni hapo amefunga mabao 38 na kutoa pasi za mwisho 10 katika mechi 58. Alijitangaza mwenyewe msimu huu kwa kufunga mabao saba na pasi za mwisho 10 kwenye Ligi ya Europa.

Hakuna mchezaji katika kikosi cha Uholanzi aliyefunga mabao mengi kwenye kufuzu Euro 2020 kama Donyell Malen. Awali alikuwa akihuishwa na klabu kubwa kama Borussia Dortmund. Kiwango chake bora kwenye Euro 2020 kinaweza kumfanya mchezaji huyo kuwania na timu kubwa.

**#1. GERARD MORENO | HISPANIA**


Ni mshambuliaji wa Villarreal na alimaliza nafasi ya pili kama mfungaji bora wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu nyuma ya Lionel Messi.

Gerard Moreno bila shaka yoyote ni mmoja wa wachezaji bora kabisa wa Hispania na katika michuano hii ana nafasi ya kung'ara. Tayari Moreno anazivutia klabu nyingi kutokana na uwezo wake dimbani na michuano hii ya Euro 2020 inaweza kumnyanyua zaidi.

Alicheza mechi nne za Hispania msimu huu kuelekea Euro 2020, tatu akitokea benchi. Hispania haipo kwenye kiwango kizuri kwa sasa, hivyo uwezo wa Moreno unaweza kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa kikosi hicho.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya soka kuweza kuibuka mfungaji bora kwenye ligi tatu kati ya tano kubwa barani Ulaya, Premier League, La Liga na Serie A, hii ni baada ya msimu huu kutwaa tuzo ya mfungaji bora Italia [Capocannoniere Trophy] kwa kufunga mabao 29.





# WACHEZAJI 10 BORA LIGI YA MABINGWA ULAYA 2020/21

N'GOLO KANTE

**NYON,** Uswisi

CHELSEA imebeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika fainali iliyozikutanisha timu za England pekee, kwa kukifunga kikosi cha kocha, Pep Guardiola, Manchester City. Ushindi wa Chelsea kwenye mashindano hayo ulikuja baada ya kiwango bora cha kocha Thomas Tuchel.

**Taji hilo limewasaidia 'Blues' hao kuwa timu ya kwanza katika historia kushinda mataji yote makubwa ya Ulaya mara mbili.**

Kai Havertz alifunga bao pekee kwenye ushindi huo wa 1-0, lakini N'Golo Kante ndiye alikuwa mchezaji bora wa mchezo huo.

Makala haya inawaangalia wachezaji 10 bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, ambao ni...

### #10. EDOUARD MENDY | CHELSEA

Edouard Mendy alikuwa na kiwango cha kuvutia sana katika msimu huu ambao ni wa kwanza hapo Chelsea na anaonekana kufuata nyayo za gwiji, Petr Cech.

Alifikia rekodi ya kutoruhusu mabao kwenye mechi nyingi katika msimu wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiifikia ile ya Santiago Canizares (Valencia) msimu wa 2000-01 na Keylor Navas (Real Madrid) msimu wa 2015-16.

### #9. KARIM BENZEMA | REAL MADRID

Real Madrid mara zote si klabu ya kumtegemea mchezaji mmoja. Msimu huu kutokana na wachezaji kama Eden Hazard na Sergio Ramos kuwa majeruhi, Kocha Mkuu Zinedine Zidane aliwategemea zaidi Karim Benzema na Thibaut Courtois ili kushinda mechi uwanjani.

Straika huyo wa Ufaransa alikuwa mfungaji bora wa 'Los Blancos' hao katika mashindano yote na alifunga mabao sita katika mashindano hayo.  Alifunga bao katika kila mechi muhimu msimu huu, akitupia dhidi ya Atalanta na Chelsea kwenye hatua ya 16-bora.

### #8. LIONEL MESSI | BARCELONA

Barcelona haijaweza kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu iliposhinda mataji matatu msimu wa 2014-15. Klabu hiyo kuendelea kumtegemea Lionel Messi ndio imekuwa sababu ya kushindwa kwenye mechi muhimu.

Messi kwa mara nyingine tena alikuwa mfungaji bora wa klabu hiyo ya Catalunya kwa msimu huu wa 2020/21 kwa mabao 30 kwenye LaLiga. Alikuwa mhusika wa mabao saba kati ya 18 ya Barcelona, akifunga matano na kutoa pasi za mwisho mbili kwenye mashindano hayo.

Alikuwa mchezaji pekee wa Barcelona kufunga kwenye hatua ya 16-bora dhidi ya Paris Saint-Germain, akifunga mabao katika mechi zote mbili wakati wakitolewa kwa uwiano wa mabao 5-2.\

### #7. JOSHUA KIMMICH | BAYERN MUNICH

Bayern Munich walikuwa wamefunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, wakifunga mabao 27 hadi kwenye robo fainali, walishindwa kutinga nusu fainali baada ya kutolewa na PSG.

Mmoja wa wachezaji wake bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu alikuwa Joshua Kimmich, ambaye alikuwa na pasi za mwisho nne na kufunga bao moja katika mechi saba.

### #6. NEYMAR | PARIS SAINT-GERMAIN

Paris Saint-Germain walifanya kila kitu na kutinga fainali ya michuano hiyo msimu wa 2019-20, lakini hawakuwa na bahati kwenye fainali kwani walifungwa na Bayern Munich.

Msimu huu walilipiza kisasi kwa kuwafunga kwenye robo fainali, huku Neymar akitoa pasi za mwisho mbili. Alifunga mabao sita msimu huu, ikiwamo 'hat-trick' kwenye mchezo wa hatua ya makundi dhidi ya Basaksehir. Lakini majeraha ya mara kwa mara yamekuwa yakimuandama zaidi.

### #5. KEVIN DE BRUYNE | MANCHESTER CITY

Kevin De Bruyne alitwaa tuzo ya nyota wa mchezo mara tatu katika mechi saba za Manchester City katika hatua ya mtoano.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, amehusika katika mabao 25 ya City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, akifunga mara tatu na kutoa pasi za mwisho nne.

Kwenye fainali aliumia kipindi cha pili na kutolewa nje wakati Man City wakifungwa na Chelsea bao 1-0.

### #4. RIYAD MAHREZ | MANCHESTER CITY

Riyad Mahrez amejipambanua mwenyewe kama mmoja wa wachezaji muhimu zaidi wa Manchester City msimu huu.

Kukosekana kwa washambuliaji na Raheem Sterling kuwa na wakati mgumu mbele ya lango kukamfanya winga huyo wa Algeria kuwa mfungaji zaidi.

### #3. ERLING HAALAND | BORUSSIA DORTMUND

Jicho la Erling Haaland kwenye goli ni kali na kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi katika kikosi chake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alitumia mechi saba tu kufunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho mbili katika mashindano hayo, lakini alikosa mechi za hatua ya makundi kutokana na kuwa majeruhi.

Alifunga katika mechi sita na nne kati ya hizo alifunga mara mbili. Mabao yake 27 kwenye Ligi Kuu yameiwezesha timu hiyo kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021/22.

### #2. KYLIAN MBAPPE | PARIS SAINT-GERMAIN

Kylian Mbappe ni jina linalotajwa sana kwa sasa katika ulimwengu wa soka.

Mshambuliaji huyo kijana alitengeneza jina lake haraka na alishinda Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora Ligue 1, baada ya kufunga mabao 27 kwa PSG, wakati wakipoteza taji kwa Lille.

Pia alikuwa mchezaji wa aina yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akifunga mabao nane.

Hat-trick yake dhidi ya Barcelona kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora, iliwahakikishia PSG nafasi ya kucheza robo fainali.

Amekuwa na ushirikiano mzuri na Neymar kwenye safu ya ushambuliaji ya PSG na alikuwa nyota wa kikosi hicho.

### #1. N'GOLO KANTE | CHELSEA

Mechi kubwa huwa zinawatambulisha wachezaji bora duniani na msimu huu, N'Golo Kante alikuwa na kiwango bora na cha kuvutia kwa Chelsea, akionyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwenye safu ya kiungo.

Mchezaji huyo alikuwa nguzo wakati Leicester City wakishinda taji la Ligi Kuu mwaka 2016 na msimu huu amekuwa muhimu kwa Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alikuwa kwenye kiwango bora zaidi kwa Chelsea msimu huu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ndiye aliyekuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye fainali.

Yote kwa yote kiwango chake ndiho kwa hakika kabisa kilichoibeba Chelsea kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu na kuibuka mabingwa.

## Nukuu

"Tumefika mwisho wa mzunguko, kwa hiyo ni sawa kwangu kuchukua likizo. Uzoefu huu mzuri na mrefu sana na Juve, utafika mwisho mwaka huu," **Kipa wa Juventus, Gianluigi Buffon, ambaye ameidakia klabu hiyo mechi 685 na timu ya Taifa ya Italia mechi 176.**



"Sijui kitakachotokea, lakini [Kylian] Mbappe atakaribishwa Real Madrid. Ni mchezaji mwenye ubora wa kila aina wa kuwa mchezaji wa Madrid kwa baadaye, natumai hivyo. Kama ataweza kuja Madrid itakuwa bora, wachezaji wote bora wanataka siku moja kuja Real Madrid," **Mshambuliaji wa Real Madrid na Ufarasa, Karim Benzema.**



"Ninaondoka nikiwa nimeinua kichwa juu na kujivunia mafanikio yangu kwenye klabu hii. Imefika wakati wa kuaga na kusema kwaherini nyote. Miaka miwili ilikuwa safari. Asanteni sana Wanasimba na kila la kheri hadi siku nyingine panapo majaliwa," **aliyekuwa winga wa Simba, Mkenya Francis Kahata baada ya kuachana na klabu hiyo.**






# MASTAA 10 NJE YA AFRIKA HATARI MICHUANO CAF

Straika hatari wa Kaizer Chiefs, Samir Nurkovic, akiwania mpira dhidi ya walinzi wa Simba, Joash Onyango na Taddeo Lwanga kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa FNB, Afrika Kusini. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kuna Watanzania bado wanaakili ya kutaka kupunguza wachezaji wa kigeni kwa sababu tu eti kuipa nguvu timu ya Taifa, Taifa Stars, walioshuhudia Ligi ya Mabingwa Afrika wameshuhudia si tu wachezaji wa klabu kutoka mataifa mbalimbali ya bara hili, bali hata Ulaya na Amerika ya Kusini.

**Wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo, Simba haikuwa na mchezaji yeyote kutoka nje ya bara la Afrika. Ingekuwa hivyo kama Mbrazil Gerson Fraga ambaye aliumia kwenye mechi za mzunguko wa kwanza dhidi ya Biashara United angekuwapo.**

Simba ilitolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa jumla ya mabao 4-3, dhidi ya Kaizer Chiefs ikifungwa mabao 4-0 ugenini na kushinda 3-0 nyumbani.

Wakati Simba ikiwa na wachezaji 10 wa kigeni kutoka nchi mbalimbali Afrika, Kaizer Chiefs na timu zingine zilikuwa na baadhi ya wachezaji si nje ya nchi yao tu, bali hata nje ya bara la Afrika.

Wachezaji kutoka nje ya Afrika kwa kiasi kikubwa ndiyo waliochangia kuwaondoa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo.

Hii ni kwa sababu klabu siku zote zinaangalia mataji na si kutengeneza timu za taifa za kwao, kwa sababu hiyo si kazi yao.

Kwenye makala haya tunawaangalia baadhi ya wachezaji kutoka bara la Afrika wanaokipiga Ligi ya Mabingwa, huku wengine timu zao zikiwa zimetolewa, twende sasa...

**#1. SAMIR NURKOVIC - KAIZER CHIEFS**

Huyu ndiye mchezaji maarufu zaidi aliyetoka nje ya bara la Afrika kwa Watanzania. Amekuwa midomoni mwa Watanzania mara baada ya kuonekana akiichezea timu yake ya Kaizer Chiefs na kufunga mabao mawili kwenye mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Simba.

Nurkovic ni raia wa Serbia anayekipiga kwenye klabu hiyo ya Afrika Kusini na amekuwa ndiye straika tegemeo kwa timu hiyo kwa sasa.

**#2. AHMED ABDELKADER - CR BELOUIZAD**

Huyu ni kipa wa kutumainiwa na timu ya CR Belouizad ambayo ilitolewa kwa mikwaju ya penalti na Esperance ya Tunisia kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Ni raia wa Ufaransa, ingawa kwa upande wa pili pia ana uraia wa nchi hiyo ya Algeria. Naye alikuwa ni mmoja wa wachezaji nje ya Afrika waliocheza Ligi ya Mabingwa Afrika.

**#3. LEANDRO SIRINO - MAMELODI SUNDOWN**

Jina lake kamili ni Leandro Gaston Sirino Rodriguez. Ni mchezaji wa Mamelodi Sundown raia wa Uruguay anayecheza nafasi ya kiungo kwenye klabu hiyo ambayo kama Simba ilitolewa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri, baada ya kuchapwa mabao 2-0 ugenini na kulazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani. Ni mmoja wa wachezaji walioipa timu hiyo ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

**#4. FEDI BEN CHOUG - ESPERANCE**

Mchezaji huyu ni kiungo mshambuliaji anayeichezea klabu ya Esperance ya Tunisia ambayo tayari iko hatua ya nusu fainali. Ni raia wa Ufaransa, ambaye pia ana uraia wa Tunisia.

**#5. KEARYN BACCUS - KAIZER CHIEFS**

Huyu ni kiungo mshambuliaji raia wa Australia. Katika kuimarisha timu yao, Kaizer Chiefs walitoka nje ya bara la Afrika na kwenda kumchomoa mchezaji huyo anayekipiga na timu hiyo, sasa ikiwa kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**#6. ANICE BADRI - ESPERANCE**

Anacheza kama winga wa kulia wa klabu hiyo konge Afrika. Huyu pia ni raia wa Ufaransa, lakini pia amechanganya na uraia wa Tunisia alitoka Ulaya na kwenda nchini Tunisia kujiunga na timu hiyo.

**#7. RICARDO SANTOS - MAMELODI SUNDOWNS**

Ni beki wa kati tegemeo kwenye kikosi cha Mamelodi Sundowns raia wa Brazil. Amekuwa mmoja wa mabeki bora kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, akiwa mmoja wa wachezaji kutoka nje ya bara la Afrika, ambaye ametoka kwao kutafuta malisho na kuipa heshima kubwa klabu hiyo Sauzi.

**#8. SOFIAN EL MOUDANE - WYDAD CASABLANCA**

Ni beki wa kati wa timu ya Wydad Casablanca ya Morocco ambayo huchezea Mtanzania Simon Msuva. Beki huyu tegemeo wa timu hiyo ni raia wa Ufaransa, timu yake ikiwa tayari imetinga nusu fainali.

**#9. LEONARDO CASTRO - KAIZER CHIEFS**

Huyu ni kiungo mshambuliaji raia wa Colombia anayekipiga klabu ya Kaizer Chiefs. Itakumbukwa huyu ndiye aliyefunga bao la nne kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika nchini Afrika Kusini, Simba ikifa mabao 4-0, ingawa alidhibitiwa kwenye mechi ya pili.

**#10. MAURICIO ALFONSO - MAMELODI SUNDOWNS**

Ni mmoja wa mastraika hatari kwenye kikosi cha Mamelodi Sundowns kama ilivyokuwa kwa Nurkovic wa Kaizer Chiefs. Mabao yake yameibeba sana timu yake hadi ilipofikia hatua ya robo fainali kwa kutokewa na Al Ahly.

**JE, WAJUA?**



MANUEL Neuer amefikia rekodi ya Oliver Kahn ya kipa aliyedaka mechi nyingi bila kuruhusu bao [clean sheets] (mechi 204). Neuer amefikia rekodi hiyo baada ya mechi 437 tu, wakati Kahn yeye alihitaji mechi 557 kuweka rekodi hiyo Bundesliga.





# TEMESA yatakiwa kubadilika kiutendaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Joseph Malongo, ameutaka Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), kubadilika kiutendaji ili kuondoa malalamiko yaliyopo kuhusu huduma zinazotolewa.

Mhandisi Malongo aliyasema hayo katika uzinduzi wa karakana sita zinazohamishika (mobile workshop), vifaa stahiki vya kuchunguza ubovu wa magari pamoja na viti 33 vya wenye mahitaji maalum kwa ajili ya kusaidia abiria wanaovuka katika vivuko vyote nchini vinavyosimamiwa na Wakala huo.

Alisema pamoja na wakala huo kuwa na karakana kila mkoa, lakini bado huduma zinazotolewa haziridhishi.

"Wakala huu umebweteka kutokana na kukosekana kwa ushindani wa kibiashara na kuwa ni Taasisi ya Serikali pekee kwenye matengenezo ya magari, nilivyoingia wizarani mwezi wa tatu, niliamua kufanya utafiti kwa baadhi ya Taasisi za Serikali kuhusu utendaji wa TEMESA, nilifanya hivyo kwa sababu nilikuwa mlalamikaji kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala huu," alisema.

Alibainisha matokeo ya utafiti wake yalionyesha asilimia 75 ya watu aliowahoji walisema TEMESA wamebweteka na pia wafanyakazi wake hawaendani na mabadiliko ya teknolojia.

"Pia utafiti ulibaini kuwa Wakala huu umetawaliwa na ukiritimba, ukosefu wa uweledi kwenye kazi na ubadhirifu wa vipuri ambapo baadhi ya vifaa vinavyofungwa katika magari si halisi na huharibika muda mfupi mara tu baada ya kupatiwa huduma," alisema.

Aliutaka kuondokana na malalamiko hayo na kuboresha usimamizi wa kifedha ambao utalenga kutoa huduma nzuri kwa wateja wao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi wa Wakala huo, Prof. Idrissa Mshoro, aliiomba serikali kupitia Wakala huo kuendelea kuajiri mafundi wa kutosha ili kuongeza idadi ya mafundi na kuwapatia ujuzi utakaoendana na mabadiliko ya teknolojia ambayo yatawasaidia kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Naye, Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Mhandisi Japhet Maselle, alisema ununuzi wa karakana zinazohamishika umelenga kusogeza huduma kwa wateja walio mbali na karakana za mikoa.

Pia alisema kutoa huduma ya matengenezo ya dharura yanayotokea maeneo yasiyo na karakana hasa magari na mitambo yanapokuwa safarini au kazini nje ya ofisi.

Kuhusu vifaa vya kuchunguza ubovu wa hitilafu za magari na mitambo, Mhandisi Maselle alisema Wakala umepanga kupeleka vifaa hivyo katika kila kituo na kufafanua kuwa vifaa hivyo vitasaidia kubaini tatizo kwa usahihi na kwa muda mfupi, kutaboresha huduma na kupunguza muda wa matengenezo ya magari na mitambo pamoja na kupunguza malalamiko ya wateja kufungiwa vipuri visivyo halisi.

Alisema zaidi ya Sh. milioni 765 zimetumika katika ununuzi wa karakana sita zinazohamishika ambazo zitagawiwa katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Mtwara, Mbeya,Tabora na Dodoma, ununuzi wa vifaa 30 vya kuchunguza ubovu na hitilafu za magari na mitambo pamoja na viti 33 vya wenye mahitaji maalum.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi) Mhandisi Joseph Malongo (wa nne kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa karakana sita zinazohamishika zilizonunuliwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wateja walio mbali na karakana za mikoa. Karakana hizo zitasambazwa katika Mikoa ya Mtwara, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Arusha na Tabora. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Skimu zote za umwagiliaji kukaguliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameiagiza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kukagua skimu zote za umwagiliaji ili kujua vikwazo vilivyopo na namna zinavyofanya kazi.

Aidha, ameitaka kuangalia namna ya kuibadilisha kuwa mamlaka ili ijiendeshe yenyewe badala kutegemea uwezeshaji wa wizara.

Bashe aliyasema hayo kwenye kikao cha pamoja na taasisi hiyo kilichojumuisha taasisi mbalimbali za wizara hiyo.

Alisema serikali inajenga na kuwekeza kwenyemiundombinu ya umwagiliaji na wataalamu lazima waweke utaratibu wa kujiuliza hizo fedha zinarudi kwa namna gani. Alisema kuwa tume hiyo inawajibu wa kutoa taarifa zote katika maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa maboresho.

"Inatakiwa wiki hii mkubaliane wenyewe na mje na wasilisho la namna ya kuzifanya hizo skimu uchunguzi ufanyike kwenye skimu zote na kuangalia nini kinatakiwa kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo," alisema.

Alisema tume hiyo inapaswa kubadilishwa muundo ili kujisimamia yenyewe.

"Siyo vizuri tuendelee kusaidia katika miradi ya umwagiliaji, serikali itaweka kidogo na wengine wawekeze, halafu unatengenezwamfumo ambao utakuwa unafanya kazi bila changamoto yoyote."

"Naiomba hii kamati iende ikatembelee miundombinu iliojengwa na miradi, na wakati mnatembelea mnapaswa kufikiria kama hizo zingekuwa za kwako ungejenga namna hiyo nakuziacha bila faida," alisema.

Alisema serikali imeanzisha mfuko wa umwagiliaji ambao umeanza mwaka huu na matarajio ni kukusanya Sh. bilioni 42 kwa ajili ya kusaidia shughuli za umwagiliaji.

"Tunatakiwa kuwa na irrigation ambayo inajitegemea, kujiendeshavizuri na kuwa na vyanzo vyake vya mapato ili taasisi iweze kujiendesha yenyewe," alisema Bashe.

Pia, alisema Wizara ya Kilimo imeamua kuweka kazi ambazo zitafanywa na Tume ya Umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kuweka nguvu katika mashamba ya Wakala wa Mbegu kwa ajili ya kupanda mbegu.

"Tunatarajia kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yote 13 ya ASA... huu ndio mkakati uliopo ili ASA aweze kufanya shughuli zake kwa mwaka mzima bila bughudha yoyote, hapa haijalishi tuna kiasi gani cha fedha, lakini ni lazima tuwekeze katika vifaa ili ifanye kazi ya kukusanya maji yanayosafiri ovyo kwa kuchimba mabwawa," alisema.

Awali, Mratibu wa mradi wa USAID wa sera bora, Prof. David Nyange, alisema kilimo chaumwagiliaji kinahitaji uwekezaji mkubwa ili kuleta maendeleo nchini.

# Vijana wapewa nafasi kampeni kutunza mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Kamati Maalumu ya Uratibu wa Kampeni ya Mazingira nchini, Seif Ali Seif, amesema katika kufanikisha kampeni hiyo ni lazima kuwajengea vijana utamaduni imara wa kutunza mazingira.

Akizungumza juzi kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira iliyoambatana na uzinduzi wa kampeni hiyo, Seif alisema ili kufanikisha hilo kampeni inapaswa kuanzisha kwenye shule hadi vyuo vikuu.

"Tunawategemea wanafunzi kufanikisha hilo, tukipanda mbegu nzuri tutapata matunda mazuri, pia elimu ya kutosha inapaswa kutolewa kuanzisha ngazi ya familia ili kuhamasisha wananchi kushiriki kutunza mazingira na si kusubiri siku ya maadhimisho," alisema.

Alisema mabadiliko ya mazingira yamesababisha vipindi vya mvua na kiangazi kushindwa kutabirika kama zamani.

"Natoa shukrani kwa serikali kwa heshima iliyotupatia sisi wajumbe 19 ambao tumekabidhiwa jukumu hili muhimu la kitaifa la kusimamia utunzaji wa mazingira," alisema.

Alisema kamati hiyo anayoisimamia inajumuisha wadau kutoka taasisi mbalimbali za serikali na binafsi, hivyo itahamasisha kila kaya, taasisi, mkoa na kitaifa kuhusu utunzaji mazingira.

"Tunaahidi kwa pamoja kushirikiana na serikali kutimiza majukumu yetu kwa weledi na uadilifu mkubwa, kampeni hii inalenga kuhamasisha katika kila kaya taasisi, kimkoa, kiwizara na kitaifa, baada ya kuhamasisha ni kuwashirikisha kuunga mkono azma hii ya mazingira kwa pamoja na kwa vitendo," alisema.

Alisema kamati hiyo itawashindanisha na kupata washindi wa kitaifa, na kwamba jukumu hilo ni zito na linatakiwa kufanikishwa kimkakati.





## Polisi yawafunda madereva sheria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi kitengo cha Usalama Barabarani mkoani Mbeya, limewataka madereva wote wa vyombo vya moto kuhakikisha wanafanya kazi hiyo kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani ikiwamo kuwa na leseni ya udereva.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Mbeya, Meloe Busema, wakati alipokuwa anazungumza na waendesha pikipiki za abiria maarufu kwa jina la bodaboda na waendesha bajaji.

Alisema madereva wengi wa vyombo hivyo wamekuwa wakisababisha ajali kutokana na kutozijua sheria za usalama barabarani na kuwataka kwenda shuleni kupata mafunzo ya udereva.

Alisema Jeshi hilo kwa kushirikiana na moja ya vyuo vya udereva jijini Mbeya, wameandaa mafunzo kwa madereva hao ili kuhakikisha wanazifahamu sheria na kuzizingatia wakati wa kuendesha vyombo hivyo ili kupunguza ajali.

"Tumeamua kuanzisha mafunzo haya ili kuwarahisishia madereva hawa kuyapata na kupata leseni, baada ya mafunzo haya hatutegemei kumuona dereva anayeendesha vyombo hivi akiwa hana leseni ya udereva," alisema Buzema.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa yenye vyombo vingi vya moto na mafunzo hayo ni muhimu akawataka hata madereva ambao tayari wana mafunzo kuhudhuria ili kukumbushwa baadhi ya misingi.

Alisema wataendelea kufanya oparesheni za kukagua vyombo vya moto na madereva ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa kufuata sheria na kupunguza ajali za barabarani.

Aliwataka viongozi wa bodaboda na bajaji kuwahamasisha wanachama wao kuhudhuria mafunzo hayo ili wafanya kazi kwa kufuata sheria na kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

# Uharibifu mazingira watishia Chunya kuwa jangwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WILAYA ya Chunya mkoani Mbeya inakabiliwa na tishio la jangwa kutokana na uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji ovyo wa miti kwa ajili ya shughuli za uchimbaji wa madini, shughuli za kilimo na uchomaji wa mkaa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Bosco Mwanginde, aliyasema hayo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya wiki ya mazingira duniani ambayo kwa wilaya hiyo yalifanyika katika Soko la Uhindini lililopo Chunya mjini.

Alisema maeneo mengi ya wilaya hiyo yameharibiwa kutokana na ongezeko kubwa la ukataji wa miti bila kupanda mingine, huku wachimbaji wa madini wakiyaacha mashimo bila kuyafukia baada ya kumaliza kuchimba.

Aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuwa na utamaduni wa kupanda miti kwenye maeneo yao ili kulinda mazingira yasiharibike kwa maelezo kuwa ndio uhai wa binadamu na viumbe wengine.

Aidha, walimu katika shule zote za wilayani humo wametakiwa kutoa elimu ya mazingira kwa wanafunzi ili kuwajengea utamaduni kundi hilo ambalo linaelewa zaidi.

"Sisi wanachunya ndio tunaongoza kwa kudharau mazingira, tunakata miti ovyo tukiamini kuwa haitaisha kwa sababu tuna misitu mingi, niwaambie tu kwamba miti hii inaisha, hii Chunya ya sasa ni tofauti na ya miaka iliyopita, hii ya sasa inabadilika inakuwa kame," alisema Mwanginde.

Aliwataka wakulima kuhakikisha wanapanda miti pembezoni mwa mashamba yao kwa ajili ya matunda na kuni ili kuepusha ukataji miti ya asili kwa ajili ya nishati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chunya, Sophia Kumbuli, aliwataka wananchi kuhakikisha kila mmoja anajenga choo bora ili kuepuka kuchafua mazingira na kusababisha magonjwa ya mlipuko ambayo yanagharimu maisha ya watu.

Aliwataka pia kushiriki kwenye usafi wa mazingira ya makazi, biashara na taasisi za umma ili kuyafanya maeneo yao kuwa masafi wakati wote.

Alisema hali ya hewa nzuri husababishwa na uwapo wa mazingira safi ikiwamo utunzaji wa misitu ambayo ndiyo chanzo cha hewa ya oksijeni ambayo humfanya binadamu na viumbe hai vingine kuendelea kuishi.

"Maingira ndio uhai wetu, kwahiyo nawaomba wananchi wote kila mmoja ashiriki kutunza mazingira ili uhai wetu uendelee kuwepo, tujenge utamaduni wa kupanda miti kwenye makazi yetu kwa ajili ya kivuli na matunda," alisema Kumbuli.

Akizungumza kwa niaba ya Idara ya wanyamapori na misitu, Ofisa wanyamapori wa wilaya hiyo, Petro Haule, alisema wakati wa maadhimisho ya siku ya mazingira duniani viongozi wa serikali na wananchi walishiriki shughuli mbalimbali za utunzaji wa mazingira.

Alizitaja baadhi ya shughuli hizo kuwa ni pamoja na upandaji wa miti kwenye maeneo mbalimbali ya umma ikiwamo katika hospitali ya wilaya pamoja na Soko la Uhindini.

Vilevile, alisema viongozi wa kata na vijiji walishirikiana na wananchi kufanya usafi kwenye vyanzo vya maji ili kuyafanya maeneo hayo kuwa rafiki kwa afya za wananchi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Sphia Kumbuli akimwagilia moja ya miti iliyopandwa katika Hospitali ya Wilaya hiyo juzi wakati wa maadhimisho ya kilele cha wiki ya mazingira duniani. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Mkandarasi aahidi kasi ukarabati MV Mbeya

NA NEBART MSOKWA, KYELA

UKARABATI wa meli ya MV Mbeya II iliyopata hitilafu baada ya kupigwa na dhoruba hivi karibuni, umeanza.

Kazi hiyo imenza, huku Kampuni ya Songoro Marine ambayo ndiyo iliyojenga meli hiyo pamoja na zingine mbili za mizigo ikiahidi kukamilisha ndani ya siku 14 zilizotolewa na serikali.

Meli hiyo ilipigwa na dhoruba katika ufukwe wa Mtema kwenye Ziwa Nyasa, wilayani Kyela ikitokea katika Bandari ya Mbamba Bay mkoani Ruvuma kuelekea katika Bandari ya Kiwira, wilayani Kyela na zaidi ya abiria 80 waliokuwamo walinusurika kifo.

Baada ya hitlafu hiyo, serikali ilisitisha safari za meli hiyo mpaka itakapofanyiwa ukarabati na tathmini pamoja na meli zote za abiria zinazofanya kazi ndani ya ziwa hilo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alifanya ziara ya kikazi hivi karibuni katika Bandari ya Kiwira na kufanya kikao maalumu na wadau wa meli na kutoa maelekezo kwa Mamlaka ya Bandari (TPA) kushirikiana na Kampuni ya Songoro Marine, kukarabati meli hiyo ndani ya siku 14.

Akizungumza na wandishi wa habari, Mkurugenzi wa Kampuni ya Songoro Marine, Salehe Songoro, alisema wameshaanza kazi ya ukarabati kwa kuanzia kuitoa kwenye maji meli hiyo na kuanza kuichunguza maeneo ambayo yameharibika.

Alisema kwa sasa ni vigumu kukadiria gharama itakayotumika kuikarabati meli hiyo mpaka watakapoifanyia uchunguzi na kubaini maeneo mengine ambayo imeharibika mbali na injini na taa ambazo zilibainika awali.

"Kuna baadhi ya maeneo tunasubiri 'tui-dock' (tuiopowe) ndiyo tutajua gharama, lakini naamini ndani ya siku 14 ambazo Naibu Waziri ametupatia tutakuwa tumemaliza kazi na wananchi wataanza kupata huduma," alisema Songoro.

Alisema kampuni yake iko imara na ina wataalamu wa kutosha ambao wana uwezo wa kuifanyia matengenezo meli hiyo haraka na kwa viwango vinavyotakiwa.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kyela waliwaomba maofisa wa TPA kuwashirikisha kwenye shughuli mbalimbali zinazohusu meli hizo ili na wao wawe na taarifa za kutosha zitakazowafanya washiriki hata kwenye uokozi.

Mbunge wa Kyela, Ally Jumbe, alisema wakati meli hizo zinajengwa wananchi wa wilaya hiyo walikuwa wanashirikishwa na ndiyo waliokuwa wanatoa ulinzi, lakini baada ya kukamilika hawajawahi kushirikishwa tena.

Alisema walishangaa baada ya kuona meli hizo zimeondolewa katika eneo hilo na kupelekwa Mbamba Bay na baadaye kusikia kupitia vyombo vya habari kwamba Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amezindua.

"Tunaomba tupewe taarifa za kutosha ikiwamo ratiba za safari za meli hizi ziwepo kwenye serikali zetu za vijiji na hata kwa Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye mwenye vyombo vya ulinzi na usalama, hii meli ilipata dhoruba bila hata Mkuu wetu wa wilaya kujulishwa," alisema Jumbe.

Naye Njohore Mwang'onda alisema wananchi wa wilaya hiyo hawajui ni nini kilichosababisha meli hiyo kupata shida huku akiwataka wataalamu kuwapa taarifa sahihi kwa maelezo kuwa kila mtu ana majibu yake.



# Othman asisitiza wananchi kutunza mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha anatunza mazingira kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani, Nyamanzi Wilaya ya Magharibi 'B', Unguja, alisema sio vyema jamii kuharibu mazingira huku jukumu la kuyatunza na kuyasimamia wakiziachia taasisi maalum au viongozi wa serikali.

Katika maadhimisho hayo yaliyoambatana na kupanda mikoko kwenye ufukwe wa Nyamanzi uliojumuisha wadau mbalimbali wa mazingira, wanafunzi na wananchi wa shehia za Nyamanzi na Dimani, Makamu huyo aliitaka jamii kuelewa athari za uharibifu wa mazingira kwa nchi.

Alisema, kama kasi ya ukataji miti na ufyekaji ovyo wa misitu haitadhibitiwa, kuna hatari ya kusababisha janga la kimazingira na kuiweka ardhi kwenye ukame, hivyo kupoteza rutuba na kudumaza kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

"Wakati nikija hapa, nilikuwa nayatazama maeneo ya Nyamanzi ya sasa nikiilinganisha na ile ya zamani. Kwa kweli utashi wetu umetufanya tukate miti na misitu katika ardhi ambayo ingefaa kwa kilimo na badala yake tumejenga nyumba," alisema.

Ingawa alikiri kuwa ujenzi wa nyumba za makazi ni jambo la msingi kwa binadamu, lakini alisema kwa bahati mbaya bado Zanzibar haijaweza kutumia ardhi ndogo kwa kujenga majengo makubwa yatakayokaliwa na watu wengi na badala yake kila mtu anakimbilia kujenga nyumba ndogo kulingana na kipato chake.

Alisikitishwa na watoto wengi wa sasa kutojua matunda yaliyokuwa mashuhuri Zanzibar akitoa mfano wa zambarau, fuu, mbura, pilipili doria na mengine, ambayo alisema yametoweka kutokana na kukatwa miti hiyo bila kupandwa mingine.

Aidha, aliwahimiza wananchi kuendeleza utamaduni wa kupanda miti katika maeneo yanayowazunguka, ili kurejesha uasili wa visiwa vya Zanzibar, ambayo miaka iliyopita ilivutia kwa rangi ya kijani kibichi iliyopambwa pia na aina mbalimbali za ndege na viumbe wengine.

Naye Dk. Saada Mkuya Salum, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema hatua ya kupanda mikoko, imelenga kutekeleza agizo la Makamu wa Kwanza wa Rais, kuwataka watendaji kujikita zaidi katika kazi za vitendo nje ya ofisi.

Alisema, miongoni mwa mambo yanayofanywa na Idara ya Mazingira kwa ustawi wa nchi, ni kuzishirikisha asasi za kiraia, wanaharakati na wanafunzi katika mikakati ya kurejesha uoto wa asili unaopendezesha mandhari ya Zanzibar.

Pia alisema, katika kuthamini juhudi za wadau na asasi hizo kutunza mazingira, maadhimisho ya mwaka huu yamehusisha kuwatunza washirika waliofanya vizuri zaidi katika uhifadhi wa mazingira.

Alisema, zawadi hizo zimelenga kuishajiisha jamii hasa makundi ya vijana na wanawake katika kutambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa vitendo.

Ujumbe wa mwaka huu kwa Zanzibar katika kuadhimisha siku hiyo ni, "Tunza mazingira kwa kurejesha uasilia wake kufikia uchumi wa bluu".



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud, akipanda mti aina ya mkoko katika fukwe ya Bahari ya Nyamanzi nje ya mji wa Zanzibar, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watakiwa kujikita kilimo cha majongoo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFUGAJI wa mazao ya baharini wametakiwa kujikita katika kilimo cha majongoo ya pwani ambacho mahitaji yake ni makubwa katika soko la nje la kimataifa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Abdalla Hussein Kombo, wakati akiwasilisha makadirio, mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021-2022 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema wizara tayari imeanza kuwashajihisha wafugaji wa mazao ya pwani ikiwamo majongoo na jumla ya wafugaji 180 wametambuliwa katika mikoa mitano ya Unguja na Pemba.

Alisema hatua hizo ni pamoja na ujenzi wa vizimba vinne vya mashamba ya mfano vyenye mita za mraba 1,800 kila kimoja kilijengwa katika bahari ya vijiji vya Mkokotoni, Kama, Shungi, Makunduchi na Chwaka.

Alisema ziara ya kuangalia maeneo yaliotengwa kwa ajili ya ufugaji wa vifaranga vya majongoo umefanyika katika kijiji cha Bungi na Kingungwi na maeneo ya ufugaji wa vifaranga umeanza.

Alisema kituo cha vifaranga kiliopo Beit-el-Ras kinaendelea na kazi za uzalishaji vifaranga hivyo kwa ajili ya wakulima walioamua kujikita katika kilimo hicho.

"Utafiti uliofanywa na wizara umebaini kwamba ufugaji wa mazao ya majongoo ya pwani hivi sasa una tija kubwa na kipato chake ni kizuri kitakachomkomboa mkulima kwa hivyo tumeanza kuwashajihisha walengwa hao," alisema.

Alisema serikali ya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mazao ya baharini ya mwani na kuongeza thamani ya uzalishaji wake.

Alisema kiwanda hicho kinatarajiwa kujengwa Chamanangwe, Pemba ambacho kitakuwa mkombozi kwa wakulima wa kilimo hicho ambao asilimia 80 ni wanawake.

Aidha, alisema katika utekelezaji wa mpango kueleekea uchumi wa bluu serikali inakusudia kujenga kiwanda cha kusarifu dagaa huko Mkokotoni pamoja na minofu ya samaki huko Malindi Unguja.

# Waomba ulinzi kudhibiti udhalilishaji kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

WAATHIRIKA wa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar, wameviomba vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha vinaimarisha ulinzi na kuwadhibiti watuhumiwa wa vitendo vya udhalilishaji kutotoroka ili kuzuia udhalilishaji mwingine unaoweza kutokea.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, waathirika hao ambao watoto wao wamebakwa na kulawitiwa (majina janahifadhiwa), walisema watuhumiwa wa matukio hayo wanapopewa dhamana hutoroka kutoka sehemu moja na kwenda nyingine.

Walisema licha ya kutoroka wengine wanapokua nje kwa dhamana, huwapa vitisho jambo ambalo linawaathiri kisaikolijia watoto waliofanyiwa udhalilishaji.

"Mimi mtoto wangu amebakwa mtuhumiwa yupo nje kwa dhamana na kesi hizi kwa mujibu wa sheria hazina dhamana sasa inakuwaje wanapewa dhamana... tunaomba dhamana isitolewe," alisema mama wa mtoto huyo.

Mwaka jana, kisiwani Pemba, mtuhumiwa Abubakari Juma Kombo (18), mwalimu wa madrasa huko Chokocho Wilaya ya Mkoani Pemba, anadaiwa kutoroka kabla ya hukumu yake kutolewa Aprili 9, 2020.

Mtuhumiwa huyo alipata hukumu ya kwenda chuo cha mafunzo miaka 12, na kulipa fidia ya Shilingi milioni nne, baada ya kupatikana na hatia ya kumlawiti mwanafunzi wake mwenye umri wa miaka sita kama ilivyosomwa na Hakimu wa Mahakama ya Mkoa Chake Chake, Abdull-razak Abdull-kadir Ali.

Inadaiwa mwalimu huyo wa madrasa alitorokea Unguja na hakuweza kutumikia adhabu yake hiyo.

Kombo ambaye sasa ana miaka (19), inadaiwa kuwa alipotoroka Pemba na kukimbilia Unguja alifanya tena vitendo hivyo vya udhalilishaji na kushtakiwa tena kwa mara ya pili.

Katika kesi yake ya pili anadaiwa kuwalawiti watoto wawili huko Shehia ya Mtopepo Darajabovu, Unguja Machi 2021.

Uchunguzi wa Nipashe uligundua kuwa kesi yake hiyo ilifunguliwa mahakama ya Mkoa Mwera, kesi namba IR52/2021, na hatimaye kesi hizo kuhamishiwa Mahakama ya Mkoa Vuga na kuripotiwa kama kesi mbili tofauti za ulawiti wa watoto hao zenye namba 75/2021 na 76/2021 na mtuhumiwa yupo rumande na kesi yake inaendelea.

Akitoa maoni yake wakati akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliomba vyombo vya ulinzi kuwa makini na watuhumiwa wa ubakaji na kuhakikisha wanabakia kwenye ulinzi mkali hadi kesi zao zinapomalizika.

Alisema kuachwa kwa watuhumiwa hao kunaweza kuleta majanga makubwa kwa vile hupenda kurudia vitendo hivyo popote walipo na kuendeleza udhalilishaji wa kijinsia na kuharibu maisha ya watoto wengi.

# Madereva 27 wafungiwa leseni kwa miezi sita

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADEREVA 27 wamefungiwa leseni zao kwa muda wa miezi sita kutokana na makosa mbalimbali ya usalama barabarani, ikiwamo mwendo kasi na kuharibu Mifumo ya Udhibiti Mwendo (GPS).

Mkuu wa kikosi cha usalama barabarani nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Wilbroad Mutafungwa (pichani), aliwafungia wakati akikagua na kutoa elimukwa madereva wa mabasi yaendayo mikoani katika kituo cha mabasi Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga.

Mutafungwa alisema hatua ya kufunga leseni hizo imechukuliwa baada ya jeshi hilo kubaini madereva hao kukiuka sheria za usalama barabarani kwa makusudi na kusababisha ajali za raia kupoteza maisha na wengine kupata majeraha kutokana na uzembe wao.



''Nimefungia leseni za madereva 27 kwa muda wa miezi sita ambao ni watovu wa nidhamu na hawataki kutii sheria za usalama barabarani hawataruhusiwa kuendesha magari yoyote kwa kipindi hicho na watakaokaidi hatua kali zitachukuliwa dhidi yao," alisema Mtafungwa.

Kwa upande wake, mkazi wa Manispaa ya Kahama, Sada Juma, alisema ajali nyingi zinazotokea zinachangiwa na madereva wa mabasi kuendesha magari wakiwa wamechoka na wakati mwingine kupata usingizi wakiwa barabarani.

Mmoja wa madereva wa mabasi ya abiria wilayani hapa yaendayo mikoani, Salumu Said, aliomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wa vyombo vya moto ambao wamekuwa wakiingiza mabasi mabovu kipindi cha likizo kwa ajili ya kujipatia fedha kwa kuwa dereva anapogoma kuendesha anaachishwa kazi.




Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, akifafanua jambo kwa viongozi wa madereva wa bajaji, daladala na bodaboda waliohudhuria uzinduzi wa kampeni ya safari salama, uliofanyika stendi kuu ya zamani mjini Iringa. **PICHA: ZUHURA ZUKHEIR**

# Uboreshaji mifumo ya usimamizi huduma mawasiliano wahimizwa

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imehimiza uboreshaji wa mifumo mbalimbali ya usimamizi wa huduma za mawasiliano ili kuhakikisha usalama na ubora.

Akizungumza katika ziara ya kutembelea mifumo hiyo kwenye Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), mkoani Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, alisema wananchi wanatarajia kupata huduma bora zenye usalama.

"Upatikanaji wa huduma bora za uhakika na salama ni jambo la msingi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na taifa," alisema Dk. Ndugulile.

Aliipongeza TCRA kwa ubunifu wa kujenga mifumo wezeshi kwa huduma mbalimbali za mawasiliano nchini, akisema uboreshaji wake ni muhimu.

Dk. Ngugulile alitembelea Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa Masafa ya Redio na Televisheni na Kituo cha Kuratibu Majanga ya Kimtandao (TZ-CERT) na kutoa ushauri wa kitaalam wa namna bora ya kudhibiti majanga ya kimtandao kwa taasisi na kampuni mbalimbali.

Waziri pia alitembelea Kituo cha Huduma kwa Wateja na kuhimiza TCRA kuendelea kushirikiana na taasisi zingine, ikiwamo Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kwenye ziara hiyo Dk. Ndugulile alipokelewa na Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari pamoja na menejimenti.

# NIT kununua vifaa vya ndege vya bil. 2.8/-

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimesaini mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ndege wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1.2 (Sh. bilioni 2.779),.

Umo pia mkataba wa upokeaji vitabu zaidi ya 10,000 wenye thamani ya Dola za Marekani 300,000 (Sh. milioni 694.912).

Mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ndege imeingia na Kampuni ya China inayojihusisha na uuzaji wa vifaa vya ndege iitwayo 'AVIC international Holding Company', na Mkataba wa ununuzi wa vitabu imeingia na Kampuni ya Mallory International Ltd.

Akizungumzia katika hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo miwili, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema ununuzi wa vifaa vya mafunzo ya ndege kutaisaidia NIT kutoa wanafunzi wenye uwezo na ubora katika masomo ya uandishi wa ndege.

Alisema pia itasaidia kutoa mafunzo yaliyobora na yenye ufanisi wa kimataifa kwa sababu kutakuwa na vifaa vyote vinavyohitajika katika kufundishia.

Prof. Mganilwa alisema: "Siyo hilo tu bali itasaidia kutoa wanafunzi wenye fani ya uhudumu ndani ya ndege, Ni vifaa vya kisasa na vya kimataifa ambavyo NIT inaenda kupokea na kukiwezesha chuo kuwa bora."

Mbali na hilo, alisema kupitia mkataba wa kupokea vifaa vya ndege itaiwezesha Watanzania kusoma masomo ya urubani hapa nchini pasipo kwenda nchi za nje.

Alisema kupokelewa kwa vifaa hivyo pia kutaitangaza Tanzania kimataifa kwani itakuwa imeanza kufundisha masomo ya urubani, hali itakayosababisha wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali kuja kusoma nchini.

Kuhusu mkataba wa vitabu, Prof. Mganilwa alisema NIT itapokea vitabu zaidi ya 10,000 vya masomo ya anga, reli pamoja na maji.

Alisema wakati huu nchi ikiwa katika ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati kama vile Reli ya Kisasa ( SGR), Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, wanafunzi wataweza kujifunza na kujisomea vitabu hivyo na kufahamu kwa undani kuhusu miradi hiyo.

# Mamia wamlilia TB Joshua

## • akihudumu miongo mitatu umaarufu uponyaji, uinjili



Hayati Dk. John Magufuli akimpokea Mhubiri wa kimataifa kutoka Nigeria, TB Joshua, kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam, Novemba 3, mwaka 2015. Mhubiri huyo aliwasili nchini kushuhudia Hayati Magufuli alipoapishwa kwa muhula wa tano wa urais. **PICHA: MTANDAO**

**Lagos,** NIGERIA

MAMIA wa waombolezaji wamemiminika mtandaoni kumlilia Mhubiri maarufu wa kimataifa wa nchini Nigeria, Temitope Balogun Joshua maarufu kwa jina T.B Joshua, ambaye ameacha ujumbe muhimu saa chache kabla ya kufariki dunia.

Ujumbe wake wa mwisho TB Joshua akizungumza kwenye Emmanuel TV Partners Meeting siku ya juzi, alisema: Ni wakati wa kila kitu, wakati wa kuja hapa kwa maombi na wakati wa kurudi nyumbani baada ya ibada.

Pia, akiwa kwenye mahubiri yake jana, Jumapili asubuhi, TB Joshua alikinukuu kitabu cha Biblia kutoka Wafilipi 4:13; Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu. Taarifa kifo chake zilianza kusambaa mtandaoni na kwenye vyombo vya habari tangu jana alfajiri, huku picha mitandaoni na video zikionyesha mamia ya waombolezaji waliokusanyika mbele ya kanisa hilo wakiomboleza.

Kanisa lake la Synagogue Church of All Nations (SCOAN), ambalo lilianzishwa na muhubiri huyo lilithibitisha habari za kifo chake, jana alfajiri. Taarifa zinasema kio chake ni muda mfupi baada ya kuongoza ibada kwenye kanisa hilo jana.

Sababu ya kifo chake hazijawekwa wazi, ingawa kwenye ukurasa wake wa Facebook wenye wafuasi milioni tano, uliandika jana: Mungu amemchukua mhudumu wake.

Umaarufu wa TB Joshua, ulianza kukua miaka ya 1990, na kufahamika kama nabii, akiongeza wafuasi dunani huku akizuru nchi mbalimbali barani Afrika, Marekani, Uingerea na Amerika ya Kusini.

Mwaka 2014, upande mmoja wa paa la kanisa lake liliporomoka na kusababisha vifo vya watu 116. Ni takribani mwezi mmoja, tangu binti yake Serah Joshua alipofunga ndoa na kijana wa Kitanzania, Brian Moshi, jijini Arusha, Tanzania, harusi ambayo ilihudhuriwa mke wa mhubiri huyo.

Maharusi hao waliteka vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii, baada ya ndoa iliyofungishwa na Padri Festus Mangwangi, Mei 8, mwaka huu, kwenye Kanisa Katoliki la Moyo Safi Mama Bikiria Maria lililopo eneo la Unga Ltd jijini Arusha.

Baada ya ndoa sherehe ilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa AICC, ikihudhuriwa na mke wa TB Joshua pamoja na ndugu zake kutoka Nigeria pamoja na familia ya bwana harusi.

### NIGERIA YAOMBOLEZA

Baada ya kutangazwa kifo chake na kuthibitishwa na kani-



sa lake, waombolezaji ikiwamo waumini wa kanisa lake SCOAN walianza kuomboleza.

TB Joshua amefariki jana, siku tano kabla ya kusheherekea siku ya kuzaliwa kwake, Juni 12.

Mmoja wa waombolezaji mtandaoni aliyejitambulisha kwa jina ojays aliandika: Mtu mkubwa ameondoka, ni tukio la kumpoteza lililo kubwa kwa kanisa. Salamu za rambirambi kwa familia na wafuasi wake.

Pia founuigbbe aliandika: Familia yake ipate faraja katika kipindi hiki kigumu. Roho yake ipumzike mahali pema peponi, Amen.

### TB JOSHUA NI NANI?

TB Joshua ni raia wa Nigeria, kiongozi na mwanzilishi wa kanisa la SCOAN ambalo hurusha matangazo yake mubashara kupitia runinga ya Emmanuel TV mjini Lagos, Kusini mwa Nigeria.

Alizaliwa Juni 12, miaka 57 iliyopita katika jimbo la Ondo, kwa mujibu wa mtandao wa kanisa la SCOAN.

Taarifa za mtandao huo zinaeleza kuwa, TB Joshua alikaa tumbo la mamake kwa miezi 15 kabla ya kuzaliwa kwake.

Joshua alisoma katika shule ya msingi ya St. Stephen Anglican Ikare-Akoko, kuanzia mwaka 1971 hadi 1977 na kisha kujiunga na masomo ya sekondari.

Akiwa shuleni alijulikana kama mhubiri mdogo kutokana na kupenda Biblia na uwezo wa kutabiri matukio yaliofanyika katika jamii yake. Alianzisha kanisa la SCOAN mwaka 1987 akiwa na waumini wachache kabla ya kanisa hilo kupanuka hadi kimataifa.

Mwaka 2009, TB Joshua alianzisha klabu ya kandanda aliyoiita My People FC katika juhudi za kuwasaidia vijana.

Wanachama wawili wa timu hiyo, Sani Emmanuel na Ogenyi Onazi, walichezea Nigeria Golden mwaka 2009, katika kombe la dunia la wachezaji wasiozidi umri wa miaka 17.

Tayari wachezaji watatu wamepata ufadhili Ulaya, kuwa wachezaji wa kulipwa nchini Sweden. Kwa mujibu wa jarida la Forbes 2011, TB Joshua ni mhubiri wa tatu tajiri nchini Nigeria, akiwa na thamani ya Dola 15 milioni.

### ALIVYOTAFSIRIWA

Baadhi ya watu walikuwa wakimkosoa kutokana na idadi ya miujiza yake anayofanya katika mikutano yake.

Baraza la Makanisa ya Pentecostal nchini Nigeria (PFN), chini ya mwavuli wa makanisa ya Pentecostal nchini Nigeria haykukubaliania na kanisa lake.

Christ Okote, mhubiri wa kanisa maarufu nchini Nigeria alimshutumu Joshua kwa kuwa ni mganga na wakosoaji wake wa Kikristo wakidai mbinu alizozitumia hazikuendana na Biblia.



Mamia ya waombolezaji wakiwa katika Synagogue Church of All Nations (SCOAN), jana. **PICHA: MTANDAO**

### UJIO WAKE TANZANIA

Novemba 3, mwaka 2015, TB Joshua aliwasili jijini Dar es Salaam ili kushuhudia kuapishwa kwa Rais wa awamu ya tano Dk. John Magufuli (hayati).

Alipowasili, alikwenda Ikulu, jijini, kumsalimia Rais mstaafu Jakaya Kikwete na kumpongeza kwa kufanikisha uchaguzi mkuu kwa uhuru na amani.

Pia, TB Joshua alipongeza Kikwete kwa kumpata Dk. Magufuli, kama mrithi wake, akimtakia Hayati Magufuli baraka na fanaka tele katika awamu yake.

Kadhalika, alifanya mazungumzo na aliyekuwa mgombea urais kwa mwaka 2015 kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Edward Lowassa.

# ALLEGRI APAMBANA KUMBAKISHA RONALDO



**TURIN,** Italia

KOCHA mpya wa Juventus, Massimiliano Allegri, ameripotiwa kufanya mazungumzo na uongozi wa kilabu hiyo juu ya hatma ya Cristiano Ronaldo.

Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 53, anakuwa kocha wa Juventus kwa mara ya pili, baada ya kufutwa kazi kwa Andrea Pirlo mwezi uliopita.

Kwa mujibu wa Goal, Juve na Allegri tayari wamefanya mkutano kujadili mipango yao ya soko la uhamisho na mustakabali wa Ronaldo ulikuwa ni kipaumbele kwenye agenda za mkutano.

Nyota huyo wa Ureno amekuwa akihusishwa sana na kuondoka kwa Juventus msimu huu wa joto, licha ya klabu hiyo kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, na klabu yake ya zamani ya Manchester United inaaminika kutaka huduma yake.

Juve wanaaminika kuwa tayari kwa kuondoka kwa nyota huyu mwenye umri wa miaka 36, ambaye anaingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake, lakini ikiwa tu ofa sahihi itatolewa.

Allegri anahitaji hali ya Ronaldo kutatuliwa haraka kwa njia moja au nyingine, na anataka ufafanuzi juu ya nafasi zipi atakazozilenga sokoni msimu huu wa majira ya joto.

Kuuzwa kwa Ronaldo kunaweza kuwasaidia Juventus kupata fedha za kuwanunua wachezaji wengine, wakiwamo kiungo wa Sassuolo, Manuel Locatelli pamoja na kuungana tena na Miralem Pjanic, ambaye kwa sasa yuko Barcelona.

# Xavi: Bado si wakati sahihi kuinoa Barca

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez amesema kuwa kupewa nafasi ya kuinoa Barcelona ilikuwa nafasi nzuri, lakini haukuwa muda sahihi wake kukubali.

Xavi aliombwa mara mbili kuchukua mikoba ya ukocha Barcelona, lakini aliamua kuitosa nafasi hiyo.

Na sasa amesema kuwa kuikataa klabu yake ilikuwa ngumu sana, lakini anahisi si wakati sahihi kwake.


"Kwa bahati nzuri au mbaya nimesema hapana kwa Barcelona mara mbili, kwa sababu ya hali tofauti, familia, mtaalamu, mkataba," alisema Xavi akinukuliwa na La Vanguardia.

"Na kwa kweli ilikuwa ngumu sana kwa sababu mimi ni shabiki wa Barcelona, lakini haukuwa wakati sahihi.

"Chochote kitakachokuja kitakuja, kitatathminiwa na tutaamua. Ofa zilifika miaka iliyopita, lakini haukuwa wakati. Barcelona ilikuja na haukuwa wakati. Hakuna haraka.

"Ninatua Barcelona, wananisubiri kwenye uwanja wa ndege na mara tu nitakapofika watu wananitumia ujumbe.

'Lakini hawajakuambia chochote?' La hasha, kwanza kwa sababu tayari wana kocha ambaye ni Ronald Koeman, lazima aheshimiwe, na pia kwa sababu mimi sina haraka."





# *Liver, Alisson kuanza kuteta*

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL inakusudia kufungua mazungumzo ya mkataba mpya na kipa wao, Alisson Becker atakaporudi klabuni baada ya msimu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kwa sasa anajindaa na michuano ya Copa America na ni miongoni mwa wachezaji ambao klabu hiyo inataka kuanza mazungumzo nao.

Alisson mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na 'Wekundu' hao kutoka AS Roma kwa mkataba wa miaka sita mwaka 2018 kwa pauni milioni 66.8.

Hiyo ilimfanya kuwa kipa ghali zaidi ulimwenguni wakati huo, na ameshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu England.

Alisson alifunga bao la ushindi muhimu dakika za jionii dhidi ya West Brom Mei na akashinda tuzo ya klabu kwa goli bora la msimu, akiwa kipa wa sita kufunga bao la Ligi Kuu England na wa kwanza kufanya hivyo kwa kichwa - Alisson ameichezea Liverpool mechi 130.

Liverpool ilikuwa na msimu mgumu baada ya kushindwa kutetea taji lao la Ligi Kuu, lakini walipata nafasi ya kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya ushindi wa 2-0 dhidi ya Crystal Palace siku ya mwisho ya kufunga msimu huu.

# Dias mchezaji bora wa msimu EPL

**LONDON,** Englad

RUBEN Dias wa Manchester City ametwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu England kwa msimu huu.

Nota huyo wa kimataifa wa Ureno, aliyejiunga na City akitokea Benfica Septemba mwaka huu, ameshinda tuzo hiyo ya pili binafsi baada ya kutajwa kuwa mchezaji bora wa msimu wa Chama cha Waandishi wa Habari wa Soka.

Aliibuka kidedea baada ya kura ya umma kuunganishwa na ile ya manahodha wa klabu 20 na jopo la wataalam wa mpira wa miguu, akiwashinda Kevin De Bruyne, Bruno Fernandes, Jack Grealish, Harry Kane, Mason Mount, Mohamed Salah na Tomas Soucek.

Dias anasifiwa sana kwa kuipatia City uimara wa beki ambao ulikosekana wakati wa msimu wa 2019-20 walipoachia taji lao la Ligi Kuu kwa Liverpool.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alishinda mechi 23 kati ya 32 za Ligi Kuu alizocheza, wakati kikosi cha Pep Guardiola kilimaliza alama 12 juu walipotwaa taji hilo kwa mara ya tatu katika misimu minne.

Alisaidia pia klabu kushinda Kombe la Carabao kwa mwaka wa nne mfululizo na kufika fainali yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo walichapwa 1-0 na Chelsea huko Porto.

Dias ndiye beki wa nne  kushinda tuzo hiyo, baada ya Nemanja Vidic wa Manchester United, nahodha wa zamani wa City, incent Kompany na Virgil van Dijk wa Liverpool.

Yeye pia ndiye mshindi wa pili wa Ureno baada ya Cristiano Ronaldo, ambaye alishinda na Manchester United msimu wa  2006-07 na 2007-08.

Ni mwaka wa pili mfululizo mchezaji wa Man City anashinda tuzo hiyo baada ya mwenzake wa Ubelgiji, De Bruyne.




# RAMOS ANUKIA MAN UTD




**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United na Manchester City imeripotiwa kuwa na nafasi ya kuipata saini ya nyota wa Real Madrid, Sergio Ramos.

Nyota huyo raia wa Hispania, mkataba wake na miamba hao wa Santiago Barnabeu unamalizika mwisho mwa mwezi huu.

Beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 35, atakuwa mchezaji huru pale mkataba wake utakapomeguka Juni 30 na kumekuwa hakuna mrejesho wowote kuhusu kupewa mpya kutoka kwa mabosi wake wa sasa.

Ripoti zimekuwa zikieleza kwamba kumekuwa hakuna mahusiano mazuri kati ya Ramos na Rais wa Real Madrid, Florentino Perez ,jambo linalomaanisha kwamba ataondoka mkataba wake utakapoisha.

Sababu nyingine ni kwamba katika orodha ya wachezaji 10 ambao hawakuwa na furaha ndani ya Real Madrid na jina la Ramos pia lilikuwamo.

Ripoti zaidi zimeeleza kuwa kutokana na janga la mlipuko wa virusi vya corona, Real Madrid inahitaji kumpa dili mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe. Ramos akiwa na Real Madrid ametwaa mataji matano LaLiga, manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ni miongoni mwa wachezaji ambao wamefanya vizuri katika kikosi hicho.

# *Conte aota mbawa Spurs*

**LONDON,** England

BAADA ya kutimuliwa kwa Jose Mourinho, ambaye tayari amepata kibarua huko Italia, safari ya Tottenham Hotspur kumsaka kocha mpya imekwama kidogo baada ya mazungumzo na Antonio Conte kuvunjika Ijumaa.

Spurs, walimtimua Mourinho Aprili mwaka huu na walikuwa kwenye mazungumzo ya kuchukua Conte ambaye ni kocha wa zamani wa Chelsea.

Lakini imefahamika kuwa madai fulani yaliyotolewa na Conte mwenye umri wa miaka 51, yamekuwa magumu na sasa wataelekeza mawazo yao mahali pengine.

Conte, alitajwa kuwa na nafasi kubwa zaidi kutokana na kuondoka kwake Inter Milan wiki iliyopita, ambapo aliondoka kwa makubaliano ya pande zote baada ya kuwaongoza kutwaa taji lao la kwanza la Serie A tangu mwaka 2010.

Rekodi yake inavutia, akiwa ameshinda pia Ligi Kuu England na Chelsea mwaka 2017, alitarajiwa kurejea Spurs kuungana na Mkurugenzi wa Juventus, Fabio Paraciti, ambaye anatajwa kuwa mbioni kujiunga na klabu hiyo.

Daniel Levy alisema alitaka klabu kurudi kwenye "DNA ya msingi" ya klabu ambayo ilipotea wakati wa uteuzi wa Mourinho.

Ripoti zinasema imekuwa changamoto kuona Conte akikidhi vigezo vya kujiunga na klabu hiyo kutokana na vipaumbele vyake alivyonavyo kwa sasa. Paraciti anatarajiwa kuwasili Spurs, na kuwa sehemu ya muhimu ya kumtafuta kocha mpya kwa ajili ya klabu yake.

Spurs pia imetajwa kuwa kwenye mazungumzo na kocha wao wa zamani, Mauricio Pochettino juu ya kurejea kwake baada ya takribani miezi 18 tu tangu kumfuta kazi, lakini mwajiri wake wa sasa Paris St Germain alizuia na itakuwa ngumu kukamilisha suala hilo tena.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO AMALIZANA NA MANCHESTER UTD

### ●●● Kuigharimu klabu hiyo pauni milioni 81 ili kukamilisha uhamisho wake huo…

**MANCHESTER,** England

GAZETI la limedai kwamba, nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, amefikia rasmi makubaliano binafsi na Manchester United.

Nyota huyo wa kimataifa wa England, ameripotiwa kufikia makubaliano hayo baada ya klabu yake kuruhusu kufanya hivyo, na sasa wakati wowote dili lake la kuondoka Dortmund linaweza kufanyika.

Dortmund wameamua kumuachia kiroho safi Sancho kuondoka klabuni hapo katika dirisha la usajili la kipindi hiki cha majira ya joto.

**Nyota huyo amekuwa akiwimdwa sana na klabu za England kwa misimu iliyopita, lakini klabu yake ilikuwa ikiweka ngumu.**

Alikaribia kujiunga na Man United miezi 12 iliyopita, lakini dili hilo kikatibuliwa dakika za mwisho kabisa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anatajwa kwamba ataigharimu Man United pauni milioni 81.5 ili kukamilisha uhamisho wake.

Sancho ambaye msimu huu hakung'ara sana, amekuwa na muda wa kuvutia kwenye Ligi Kuu Ujerumani, tangu alipojiunga na kikosi hicho.

Mchezaji huyo ambaye ni zao la akademi ya Manchester City, pia alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu yake hiyo ya zamani.

## ZISIKUPITE

### SPURS WAMTAKA TEN HAG

TOTTENHA itafanya mazungumza zaidi na kocha wa Ajax, Erik ten Hag mwenye umri wa miaka 51, baada mpango wa kumchukua Antonio Conte kushindikana. ***(Mirror)***

### FERGUSON AIKATAA MADRID

DUNCAN Ferguson amekataa nafasi ya kwenda kwenye benchi la ufundi la kocha Carlo Ancelotti pale Real Madrid kwa sababu anakata kuwa kocha wa Everton. ***(Sun)***

### MOYES KUJIFUNGA WEST HAM

WEST Ham inajiamini kwamba, David Moyes atasaini mkataba wa muda mrefu baada ya mazungumzo na kocha huyo mwenye umri wa miaka 58, ambaye amekuwa akihusishwa na kutaka kurudi Everton. ***(Football Insider)***

### TRIPPIER AITAKA UNITED

MLINZI wa kulia wa Atletico Madrid, Kieran Trippier, mwenye umri wa miaka 30, amewaambia wachezaji wenzake wa England kuwa anataka kujiunga na Manchester United kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### WIJNALDUM KUPEWA OFA

BARCELONA wanafikiria kutengeneza ofa nzuri zaidi kwa kiungo wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum, mwenye umri wa miaka 30, ambaye anapanga kuondoka Liverpool kwa uhamisho huru, baada ya Paris St-Germain nayo kuwania saini yake. ***(Marca)***

### MORIBA KUPEWA MKATABA

WIKI hii Barcelona itampa ofa ya kuongeza mkataba wa muda mrefu, mchezaji wake kinda, Ilaix Moriba mwenye umri wa miaka 18 ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwakani na amekuwa akihusishwa na Manchester City na Manchester United. ***(Marca)***

### MOURINHO ATAKA KIPA MPYA

KOCHA mpya wa Roma, Jose Mourinho, anataka kumsajili mmoja wa magolikipa wa Tottenham na Ufaransa, Hugo Lloris mwenye umri wa miaka 34, kipa wa Juventus na Poland, Wojciech Szczesny, 31, au kipa wa Wolves na Ureno, Rui Patricio mwenye miaka 33. ***(La Gazetta dello Sport)***

### XHAKA AWANIWA ROMA

KIUNGO wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28, bado anawaniwa na AS Roma. ***(Corriere dello Sport)***

### MKATABA MPYA KWA DYCHE

KOCHA, Sean Dyche mwenye umri wa miaka 49, anatarajiwa kusaini mkataba mpya na klabu ya Burnley. ***(Mail)***

### NKETIAH KUSAJILIWA

LEEDS wamepewa nafasi ya kumsajili, Eddie Nketiah kipindi hiki cha majira ya joto kwa pauni milioni 20. (***Football Insider)***

# HABARI MICHEZO

## Chirwa anogewa Ligi Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

HUKU mkataba wake ukielekea kumalizika mwishoni mwa msimu huu, straika wa Azam FC, Obrey Chirwa, amesema anaamini bado ataendelea kubaki kucheza soka nchini Tanzania msimu ujao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Chirwa mchezaji wa zamani wa Yanga, alisema yeye anajua kuwa mkataba wake unamalizika, lakini bado anaipa nafasi timu yake hiyo kwa ajili ya mkataba mpya, ila kama ikishindikana timu zipo nyingine nchini Tanzania.

"Suala la mkataba nawaachia viongozi. Mimi mwenyewe najua kuwa unakwisha, lakini naona bado nina nafasi kwa sababu mimi ni mzoefu sana na soka la Tanzania, nimecheza misimu mingi na nalifahamu, hivyo naamini Mungu akijaalia nitabaki Azam, lakini kama hakupenda basi timu hapa nchini zipo nyingi, nitaenda timu nyingine. Lakini kwanza kabisa naipa kipaumbele timu yangu ya Azam," alisema Chirwa.

Kwa maelezo haya ni kwamba Chirwa ana asilimia kubwa ya kubaki kucheza soka nchini Tanzania, ama kwa kuongezewa mkataba na klabu yake na kama sivyo basi ni wazi kuna timu za hapa hapa ambazo zinaonekana kumhitaji na yeye pia akitamani kuendelea kucheza soka Bongo.

Raia huyo wa Zambia alijiunga na Azam mwaka 2018 akitokea Nogoom FC ya Misri ambako aliyojiunga nayo muda mfupi tu baada ya kuondoka Klabu ya Yanga.

Chirwa alijiunga na Yanga mwaka 2016 akitokea Klabu ya FC Patinum ya Zimbabwe na kuichezea kwa misimu miwili kabla ya kutimkia Misri, baadaye kuibukia Azam FC, ingawa kwa sasa amekuwa hapati sana nafasi ya kucheza chini ya Kocha Mkuu Mzambia mwenzake, George Lwandamina.

MABINGWA...




Wachezaji wa timu ya wasichana Bulls U-13, wakishangilia baada ya kutwaa ubingwa kwa kuifunga timu ya Shule Msingi Feza, katika michuano ya Dar Youth Cup, iliyofanyika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# YANGA YATOA MSIMAMO USAJILI MAINGIZO MAPYA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umeweka wazi kuwa hautafanya mabadiliko makubwa ndani ya kikosi chao kwa kusajili wachezaji ambao watasaidia timu yao kufikia malengo ya kufanya vizuri kwenye michuano iliyopo mbele yao ikiwamo kutwaa ubingwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema kwa sasa wanasubiri mapendekezo ya benchi la ufundi kuhakikisha wanafanya usajili wa wachezaji kulingana na mahitahi ya timu yao kuelekea kufanikisha malengo yao.

**Alisema wanasubiri ripoti ya Kocha Mkuu Nasreddine Nabi kuona mapendekezo ya wachezaji ambao anawahitaji kwa ajili ya kuboresha kikosi chake kwa msimu ujao wa michuano itakayowakabili.**

"Viongozi hatutapelekeshwa na maneno, tutafanya usajili kwa kufuata utaratibu ikiwamo kusubiri ripoti ya kocha wetu (Nabi), kwa kuona aina ya wachezaji ambao anaowahitaji kwa ajili ya kuboresha kikosi cha timu yetu kwa msimu ujao.

"Msimu uliopita tulifanya usajili bila kuwapo kwa kocha mkuu, ila msimu huu nina imani tutasajili wachezaji tukiwa na benchi la ufundi lililokamilika," alisema Mfikirwa.

Alisema hawatafumua kikosi zaidi ya kuboresha katika nafasi ambazo zinakuwa na upungufu kulingana na mapendekezo ya usajili ambayo yatatolewa na kocha huyo.

Kwa misimu miwili mfululizo, Yanga imekuwa ikifumua karibu kikosi chote na kusajili nyota wapya huku pia wakati wa dirisha dogo ikiongeza wengine, jambo ambalo limekuwa likiwagharimu kuweza kuzoeana mapema.



Mkuu wa Kitengo cha Masoko cha Benki ya Stanbic Tanzania, Desideria Mwegelo (Kulia), akikabidhi jezi kwa Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (Taswa SC), Majuto Omary. Benki hiyo imegharamia vifaa vya michezo kwa timu hiyo, na kutoa fedha kwa ajili ya ziara ya jijini Dodoma kucheza mechi dhidi ya timu ya Bunge FC. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Stanbic yaibeba Taswa SC*

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania, imetoa msaada wa vifaa na fedha wenye thamani ya Sh. milioni 9.2 kwa klabu ya Waandishi wa Habari za Michezo nchini, Taswa SC.

Taswa SC inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya Bunge FC ambapo Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa benki ya Stanbic Tanzania, Desideria Mwegelo, amesema msaada huo utafanikisha vema ziara hiyo ya jijini Dodoma.

Mwegelo alisema benki yao inatambua mchango wa Taswa SC katika maendeleo ya michezo nchini pamoja na masuala ya afya.

"Michezo ni moja ya njia ya kujenga afya ya mwili katika jamii. Benki yetu mbali ya kusaidia michezo, pia inasaidia masuala ya afya, tunaamini kwa msaada huu, timu itafanya vizuri katika mchezo huo," alisema Mwegelo.

Alisema benki yao inajisikia fahari zaidi kushirikiana na Taswa SC kwa kuwa hufanya hivyo hiyo ikiwa ni mara ya pili.

"Msaada huu pia ni sehemu ya Benki ya Stanbic Tanzania kujishughulisha na shughuli za kijamii. Tunawaomba wachezaji wa Taswa SC watuwakilishe vizuri siku ya mchezo huo," alisisitiza Mwegelo.

Mwenyekiti wa Taswa SC, Majuto Omary, aliipongeza Benki ya Stanbic Tanzania kwa msaada huo ambao utwafanya kufanya safari yao kwa uhakika zaidi mbali ya kucheza mechi hiyo.

Majuto alisema klabu hiyo ilikuwa njiapanda kusafiri kwenda Dodoma na kwamba msaada huo umewahamasisha wachezaji kufanya vema.

"Msaada umekuja wakati muafaka ambapo klabu ilikuwa inahitaji kusafiri na kucheza mechi dhidi ya timu ya Wabunge. Naishukuru sana kwani ndoto yetu ya miaka mingi kucheza na Bunge FC jijini Dodoma itatimia," alisema Majuto.

Michezo
Jumatatu Juni 7, 2021
Nipashe



Sancho amalizana na Man Utd UKURASA 22

YALAAAH!...




Mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, akichezewa madhambi na kiungo wa Albania, Lorenc Trashi, kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Cardiff City juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: MTANDAO**

## Kipenga uchaguzi Mkuu wa TFF chapulizwa rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

KIPENGA cha kuwania uongozi wa juu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kimepulizwa rasmi baada ya kutangazwa siku ya kuanza kuchukua fomu za kuwania nafasi mbali kwenye uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Agosti 7, mwaka huu jijini Tanga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Wakili Kiomoni Kibamba, nafasi zinazogombewa ni Rais wa TFF na Wajumbe sita wa Kamati ya Utendaji.

"Fomu zitaanza kutolewa kuanzia Jumanne Juni 12, mwaka huu na zinapatikana katika Ofisi za TFF na kwenye tovuti ya TFF, kwa Sh. 500, 000 kwa nafasi ya rais na Sh. 200,000 kwa nafasi ya Kamati ya Utendaji," ilieleza taarifa hiyo.

Tayari Rais wa TFF wa sasa, Wallace Karia, alishatangaza dhamira yake ya kutetea nafasi yake katika uchaguzi huo ujao ili kurejea kuendeleza mafanikio yake katika soka la Tanzania.

# YANGA: HATUTAKI SIMBA ITUBEBE MICHUANO CAF

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Yasema itacheza Shirikisho Afrika kwa kutoa vichapo Kombe FA na kubeba 'ndoo' hiyo...

WAKATI mashabiki wa Simba na viongozi wa klabu hiyo wakijivunia juhudi zao za kuiwezesha Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa msimu ujao, Klabu ya Yanga imesema itashiriki mashindano hayo kwa msuli wao na si kupitia nafasi zilizotengenezwa na watani wao hao wa jadi.

**Kufanya vizuri kwa Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kumeiwezesha Tanzania kushika nafasi ya 12 katika viwango vya CAF, hivyo kuwa kati nchi 12 zitakazoingiza timu nne kwenye michuano ya shirikisho hilo; Ligi ya Mabingwa mbili na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.**

Hiyo ni baada ya kufikisha pointi 27.5 ikiiacha mbali Senegal inayoshika nafasi ya 13 kwa pointi 15, hivyo sasa timu mbili zitaongezeka msimu ujao kutoka moja iliyokuwa ikishiriki Ligi ya Mabingwa na moja Kombe la Shirikisho.

Katika msimu wa 2017/18, wakati Yanga ilipokuwa ikiiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa, iliambulia kuvuna pointi moja tu, lakini msimu wa 2019/20, Simba ikaiwezesha nchi kupata pointi tisa kisha msimu huu ikiongeza pointi 15 baada ya kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, wakati Namungo iliyotinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho msimu huu ikiiongezea Tanzania pointi 2.5.

Na kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), bingwa wa Ligi Kuu Bara, huiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati mshindi wa FA Cup, hubeba jukumu la kuipeperusha bendera ya nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Lakini kutokana na kuongezeka kwa timu na kuwa nne, mshindi wa pili wa Ligi Kuu ataongozana na bingwa kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa huku timu itakayoshika nafasi ya tatu ikiambatana na mshindi wa FA Cup kwenda kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Tayari Simba ipo katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kutokana na kuwa na pointi 67, sita mbele ya Yanga iliyopo nafasi ya pili huku ikiwa mbele michezo miwili na Azam ikishika nafasi ya tatu na alama zake 60 baada ya kushuka dimbani mara 30.

Hivyo, kutokana nafasi hizo ambazo Simba imezitengeneza, mashabiki na viongozi wa klabu hiyo wanaamini timu mbili zitakazoshiriki michuano hiyo kama si kwa njia ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ama Kombe la FA, zitakuwa zimekwenda kwa mgongo wao.

Lakini Mkurugenzi wa uwekezaji wa Gsm, ambao ni wadhamini wa Klabu ya Yanga, Injinia Hersi said, amesema wana uhakika wa kutwaa Kombe la FA na kwenda kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika pasipo kutegemea nafasi hizo zilizotengenezwa na Simba.

"Hatuiandai Yanga kwa kuiangalii Simba, hatutegemei pia mtu kucheza mashindano ya CAF, haijalishi wametengeneza nafasi ngapi, sisi tutaifunga Biashara na kucheza fainali.

"Mshindi kati ya Simba na Azam tutamfunga fainali na kutwaa Kombe la FA na kwenda kucheza Kombe la Shirikisho Afrika bila kumtegemea mtu yeyote," alisema Hersi.

Aidha, alisema pia anajivunia mambo makubwa ambayo Yanga imefanikiwa ikiwamo kutwaa Kombe la Mapinduzi mbele ya mahasimu wao, Simba.

Yanga itacheza nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Biashara United wakati Simba ikicheza dhidi ya Azam FC na washindi wa mechi hizo mbili watakutana fainali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >